

مَنْ هُمُ الشَّيْعَةُ وَمَنْ هُمُ أَهْلُ السُّنَّةِ ؟

MASHIA NI AKINA NANI
NA
AHLUS SUNNAH NI AKINA NANI?

Mtunzi:

Abdullaahi Ibn Muhammad

Tarjama

Abu Halima Arafat

Utangulizi

Kila sifa njema anastahiki Allaah, Swala na Salamu zimshukie Mtume wetu Muhammad, Jamaa zake, Maswahaba wake, na Yule atayewapenda hao.

Baada ya hayo: Niliandika Risala fupi kuwafahamisha waislamu itikadi za baadhi ya makundi potofu ambayo huzingatiwa ni katika waislamu, Risala niliyoiita: **[Ni Nani Shia Ithnaasharia?]**, na hilo ni kabla ya miaka kumi na mbili iliyopita, malengo yangu makuu katika Risala hiyo ni kubainisha itikadi za Shia Imaamiyyah kwa ufupi sana, baada ya kuona watu wengi hawapendi kusoma (vitabu vikubwa). Katika risala hiyo nimetaja itikadi za Mashia na kugemeza kwenye vitabu vyao vya kutegemewa, bila kusahau kutaja jina la mtunzi wa kitabu husika, juzuu na ukurasa wa kitabu hicho. Hakika Risala hiyo (kwa fadhila za Allaah) imepata mwikio mzuri kote duniani, kwa watu wa kawaida na wasomi, na (Alhamdulillah) imetafsiriwa katika lugha zaidi ya kumi na tano. Kisha ikanibainikia mimi kwamba baadhi ya wasomi wa kitabu hicho (watu wa kawaida) wanahitajia zaidi kujua itikadi za Ahlus Sunnah katika hayo ambayo Shia wameyapotosha, hilo ni baada ya kuashiriwa na ndugu yangu aliye mbora (Allaah amlipe kheri), nikaanza kupanua fikra katika kuandika kitabu hiki, kwa sifa ya kuwa kila ninapoitaja itikadi potofu ya Shia nafuatishia kutaja itikadi sahihi ya Ahlus Sunnah wal-Jamaa'h pamoja na kutaja dalili.

Kwa hiyo nimebadili anuani ya kitabu badala ya: **[Ni nani Shia Ithnaasharia?]** na kuwa: **[Mashia ni akina nani na Ahlus Sunnah ni akina nani?]**, katika kitabu hiki nimejilazimisha kutaja itikadi za Ahlus Sunnah kwa ufupi nikitilia nguvu kwa dalili katika Qur'an na Sunnah juu ya ufahamu wa Salaf, kwa hiyo kitabu hiki kinafaa kwa watu wa kawaida, wasomi na wale wanaowakosoa mashia, kwani kimeandikwa kwa lugha nyepesi iliyo wazi. Ninamuomba Allaah Subhaanah awanufaishe kwa Risala hii Waislamu, na awazindue Ahlus Sunnah kwa kuwaongoza kwenye itikadi sahihi na kuwatoa kwenye itikadi potofu. Swala na Salamu zimshukie Mtume wetu, Jamaa zake, na Maswahaba wote.

Abdullaah Bin As Salafi (Allaah amsamehe Yeye, Wazazi wake na Waislamu wote).

Riyadh -Saudi Arabia.

1. ASILI YA YA ITIKADI ZAO:

- **Mashia wanakiri na kukubali kwamba:** [Asili ya Ushia unatokana na Myahudi Abdullaahi Ibn Sabai, na kwamba Ally Bin Abi Twalib-Allaah amridhie- aliwachoma (wafuasi wake kwa moto) na akajitenga nao]⁽¹⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema kwamba:** Asili ya Dini yetu imechukuliwa kutoka kwenye Qur'an na Sunnah, hatumuabudu Allaah isipokuwa kutoka kwenye viwili hivyo. Amesema Allaah:

﴿وَمَا اخْتَلَفْتُمْ فِيهِ مِنْ شَيْءٍ فَحُكْمُهُ إِلَى اللَّهِ ذَلِكُمُ اللَّهُ رَبِّي عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَإِلَيْهِ أُنِيبُ﴾

“Na mkikhitafiana katika jambo lolote, basi hukumu yake ipo kwa Allaah. Huyo Allaah ndiye Mola wangu Mlezi, Yeye tu nimetegemea na kwake ninarejea”⁽²⁾.

Na kauli ya Mtume-Swala na Salamu zimshukie-: “Nimekuachieni nyinyi vitu viwili hamtapotea muda wa kuwa mmeshikamana navyo; Kitabu cha Allaah na Sunnah za Mtume wake”.

- **Shia wanakubali na kukiri kuitwa kwa jina la Raafidhwa.** Wamepokea kutoka kwenye jawabu la Abu Abdillaahi wakati alipoulizwa (kuhusu kuitwa kwa jina la Raafidhwa), akasema: [Hamjaitwa jina hilo na wao isipokuwa Allaah ndiye amewaita hivyo]⁽³⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunna tunasema:** Allaah ametuita sisi kuwa ni Waislamu:

﴿هُوَ سَمَّكُمْ الْمُسْلِمِينَ مِنْ قَبْلُ وَفِي هَذَا لِيَكُونَ الرَّسُولُ شَهِيدًا عَلَيْكُمْ وَتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ﴾

“Yeye (Allaah) alikuiteni Waislamu tangu zamani, na katika hii (Qur'an) pia, ili awe Mtume shahidi juu yenu, na nyinyi muwe mashahidi wa watu”⁽⁴⁾.

Maana yake: “Amewaita nyinyi kuwa ni Waislamu, ndani ya vitabu vilivyotangulia kabla ya kushuka hii Qur'an, na pia ndani ya hii Quran”⁽⁵⁾.

¹- Tazama: [Firaqi Sshia] (Uk. 22). Cha An Naubakhti na [Ikhtiyaaru ma'rifati Rrijaal] (Uk. 107) cha At Tusi.

²- Surat As Shuura/10.

³- Kitabu: [Bihaarul Anwaar] cha Al Majlis (Jz. 65, Uk. 97).

⁴- Surat Al Hajji/78.

⁵- Kitabu: [Tafsiri At Twabari] (Jz. 18, Uk. 692) na [Al Baghwi] (Jz. 3, Uk. 355).

2. ITIKADI YA MASHIA KUHUSU ALLAHAH:

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Sisi hatukusanyiki pamoja nao (Ahlus Sunnah) kuhusu Allaah, Mtume wake, wala kwa Imam, kwa sababu wao (Sunni) wanasema kwamba: Mola wao ni yule ambaye Mtume wake alikuwa Muhammad, na Khalifa wake baada yake ni Abubakar, na sisi hatumkubali Mola huyo wala Mtume huyo, lakini sisi tunaitakidi kwamba Mola ambaye Khalifa wa Mtume wake ni Abubakar huyo si Mola wetu, wala Mtume huyo si Mtume wetu]⁽⁶⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Hatukusanyiki pamoja na Shia Raafidhwa ambao hawamkubali Allaah (Mola wetu), wala Mtume wetu-Swala na Salamu zimuendee-, wala hawamkubali Abubakar ambaye ni Khalifa wake. Bali sisi tunamuamini Allaah hali ya kuwa peke yake, tunasadikisha Utume wa Mtume wake Muhammad - Swala na Salamu zimuendee- na tunakiri na kukubali Ukhalifa wa Abubakar Swiddiq ambaye alipewa Bai'a (kiapo cha utiifu) na Maswahaba wote.
- **Shia Ithnaasharia wanaitakidi kwamba:** [Mtu mwenye kuzuru kaburi ni lazima kulielekea kaburi hilo, hata kama kaburi hilo haliko upande wa kibla, kwa sababu kulielekea kaburi kwa mtu mwenye kuzuru ni sawa kama ameelekea upande wa kibla, na huo ndio upande wa Allaah ambao ameamrisha watu kuelekea]⁽⁷⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah Wal-Jamaa'h tunasema:** Ni wajibu katika swala za faradhi kuelekea upande wa kibla, (isipokuwa kwa dharura zinazotajwa katika vitabu vya fiqhi).

Allaah anasema:

﴿قَوْلَ وَجْهَكَ شَطْرَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَحَيْثُ مَا كُنْتُمْ فَوَلُّواْ وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُ﴾

“Basi elekeza uso wako upande wa Msikiti Mtakatifu, na popote mnapokuwa zielekezeni nyuso zenu upande huo”⁽⁸⁾.

⁶- Kitabu: [Al Anwaaru Nnu'maniyyah] cha Ni'matullaahi Al Jazaairiy (Jz. 2, Uk. 278).

⁷- Kitabu: [Bihaaru al Anwaar] (Jz. 101, Uk. 369).

⁸- Surat Al-Baqara/144.

Ama swala za sunnah si wajibu kuelekea upande wa kibla ikiwa mtu (yupo juu ya kipando) na hakupata yeye wepesi wa hilo.

- **Shia Ithnaasharia wanaitakidi kwamba:** [(Aah: آه)⁽⁹⁾ ni jina miongoni mwa majina ya Allaah yaliyo mazuri, yule atakayetamka jina hilo atakuwa ameomba ulinzi kwa Allaah]⁽¹⁰⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Hatumuiti Allaah isipokuwa kwa jina ambalo amejitita yeye mwenyewe au amemuita yeye Mtume wake -Swala na Salamu zimshukie-, kama inavyotajwa na kukaririwa katika itikadi ya Salaf (wema waliotangulia).
- **Shia Ithnaasharia wanaitakidi kwamba:** [Allaah anamtembelea Hussein Bin Ally -Allaah amridhie- na kumpa mkono kisha anakaa pamoja naye kitandani]⁽¹¹⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Tunajitakasa kwa Allaah na itikadi hii potofu, na tunaamini kwamba Allaah amelingana sawa juu ya 'Arshi yake, wala hafanani na viumbe wake, na yeyote mwenye kumfananisha Allaah na viumbe amekufuru, kwa kauli ya Allaah:

﴿لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ﴾

“Hapana kitu chochote ni mfano kwake yeye. Naye ni Mwenye kusikia Mwenye kuona”⁽¹²⁾.

Na kauli yake Allaah:

﴿وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُوًا أَحَدٌ﴾

“Na hakuna kitu chochote ni mfano juu yake”⁽¹³⁾.

⁹- Jambo hili nimelifafanua kwenye Makala yangu niliyooita: [Je, ni kwa akili gani na dini gani kujaalia sauti ya kuugua Aah آه ni katika majina ya Allaah?] wakati tukimjibu mmoja wa masheikh wa Kisufi (tawariqa).

¹⁰- Kitabu: [Mustadrak al Wasaail] cha An Nuuri Ttwabarsi, (Jz. 2, Uk. 148).

¹¹- Kitabu: [Swahiifat al Al Abraar] cha Muhammad Taqiy, (Jz. 2, Uk. 140).

¹²- Surat Al Shuura/11.

¹³- Surat Ikhlāas/4.

3. KAULI YAO KUHUSU KUPOTOSHWA KWA QUR'AN:

➤ **Shia Ithnaasharia wanaitakidi kwamba:** [Qur'an tukufu -hii tulionayo- imepotosha na kupunguzwa, na kwamba Qur'an sahihi anayo Mahdi wao (Imam wa kumi na mbili) aliyejificha pangoni]. Na miongoni mwa Maulamaa wao wakubwa wanye itikadi hii:

1. Ally Ibrahim Al Qummi.
2. Muhammad Bin Yaqoub Al Kulaini.
3. Muhammad Bin Nu'maan Al Mufid.
4. Muhammad Al-'ayyaash.
5. Ni'matullahi Al-jazaairiy.
6. Al-faidhul-Kaashaniy.
7. Ahmad Twabarsi.
8. Muhammad Baqir Al Majlis.
9. Abul Hassan Al-'aamiliy Adnan Al Bahraaniy.
10. Yussuf Al-bahraaniy.
11. An-nuuri At-twabarsiy.
12. Habibullaahi Al-khuui. Na wengine wengi ambao hatuwataja⁽¹⁴⁾.

▪ **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Qur'an imelindwa na kutozidishwa wala kupunguzwa, na hakika Allaah amechukua ahadi ya kuilinda Qur'an, hii, amesema Allaah Ta'alaa:

﴿إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ﴾

“Hakika sisi ndio tumeiteremsha Qur'an hii, na hakika sisi tutailinda”⁽¹⁵⁾.

Na kauli yake Allaah:

﴿بَلْ هُوَ قُرْآنٌ مَّجِيدٌ ** فِي لَوْحٍ مَّحْفُوظٍ﴾

“Bali hii ni Qur'an tukufu ** Katika ubao Ulio Hifadhiwa”⁽¹⁶⁾.

¹⁴- Kitabu: [As Shia Ithnaasharia watahriifu Qur'an] cha Muhammad As Seif.

▪ [Mauqifu Raafidhwa Minal Quranil Karim] cha Maamadu Kaarambiiliy.
▪ [Faslul khitwaab Fii Tahfrifi Kitaabi Rabbil Arbaab] cha Muhammad Habib.

¹⁵- Surat Al Hijr/9.

¹⁶- Surat Al Buruuj/21-22.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Neno: (Aal Muhammad- آل محمد na Aal Ally- آل علي), yameondoshwa ndani ya Qur'an]⁽¹⁷⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Hakika Qur'an haijapungua kitu chochote, na mwenye kuitakidi hivyo atakuwa ameipinga kauli ya Allaah na pia ameikataa Ijmaa (maafikiano ya Waislamu wote) - Allaah atukinge na hilo-:

Allaah anasema:

﴿إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ﴾

“Hakika sisi ndio tulioteremsha Quran hii, na hakika sisi ndio tutaaulinda”⁽¹⁸⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanaitakidi kwamba:** [Hakuna aliyeikusanya Qur'an yote isipokuwa (Maimamu 12 wa Kishia), na kwamba hao (Maimamu) wanajua elimu yote ya Qur'an]⁽¹⁹⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Qur'an imekusanywa na Maswahaba -Allaah awaridhie-: na kauli inayosema kwamba imedhibitiwa na Ally Bin Abi Twalib na watu wa nyumbani kwake, hayo ni maneno ya batili, na hakuna anayeamini hivyo isipowa ni Shia Imaamiyyah pekee.
- **Shia wanaitakidi kwamba:** [Kuna sura inaitwa surat Al-wilaya inaanza kwa kusema: (يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا بِالتَّوْرِينَ) [Enyi mlioamini zikubalini nuru mbili], ambazo ameziangusha Uthman Bin 'Affaan (wanavyodai)]⁽²⁰⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunaitakidi kwamba:** Qur'an imekamilika wala haijapunguzwa, kwa sababu Allaah amechukua dhamana ya kuwa atailinda hiyo Qur'an, wala hakuna yeyote anayeweza kuongeza kitu kwenye Qur'an, si Sura, Aya, wala herufi, kwauli yake Allaah:

¹⁷- Kitabu: [Minhaaju al-Baraa'h] cha Habibllaahi Al-Khuuiy (Jz. 2, Uk. 216).

¹⁸- Surat Al Hijr/9.

¹⁹- Kitabu: [Usuulu Kaafi] (Jz. 1, Uk. 228).

²⁰- Kitabu: [Faslul khitwaab fiy Tahriif kitaabi Raabil Arbaab] cha At Twabarsi (Uk. 18).

﴿ إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ ﴾

“Haika sisi ndio tulioteremsha Qur'an hii, na hakika sisi ndio ambao tutailinda”.

Na jambo hili wamekubaliana Maulamaa wote wa zamani (Salaf) na waliokuja baadae (Khalaf).

- **Shia Ithnaasharia wanasema kwamba:** Kuna msahafu unaitwa Mus-haf Faatima (Msahafu wa Fatma), na kuna ndani yake mfano wa Qur'an yetu hii mara tatu⁽²¹⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Kwamba wamekubaliana umma wote juu ya kwamba msahafu huu uliopo mikononi mwetu, ndio Qur'an tukufu ambayo Allaah alimteremshia Muhammad-Swala na Salamu zimshukie-, Qur'an ambayo imeanza kwa Surat Al Fatiha na kumalizia kwa Surat An Naas, na kwamba huo unaoitwa msahafu wa Fatma-Allaah amridhie- ni uwongo tu uliobuniwa.

4- SHIA WAMEPOTOSHA MAANA KATIKA KAULI YA ALLAAH:

﴿ بَلِّغْ مَا أُنْزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ وَإِنْ لَمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَّغْتَ رِسَالَتَهُ ﴾

“Fikisha ulioteremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi. Na ikiwa hukufanya hayo basi hukufikisha ujumbe wake”⁽²²⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanaitakidi na kusema kwamba:** Katika Aya hii kuna neno limeondoshwa, ukamilifu ni kusomwa:

﴿ بَلِّغْ مَا أُنْزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ - فِي عَلِيٍّ - وَإِنْ لَمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَّغْتَ رِسَالَتَهُ ﴾

“Fikisha ulioteremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi -**kuhusu Ally**-. Na ikiwa hukufanya hayo basi hukufikisha ujumbe wake”.

Kwa hiyo wamezidisha neno: **!!(فِي عَلِيٍّ)** kwa madai kwamba Mtume-Swala na Salamu zimshukie- hakulisema neno hilo kwa kuchelea wanafiki (wasije wakamuua Ally Bin Abi Twalib).

²¹- Kitabu: [Usuulul Kaafi] cha Al Kuleyn (Jz. 1, Uk. 239).

²²- Surat Al Maaida/67.

- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Huko ni kupotosha maana iliyokusudiwa na Allaah, na kumtia dosari Mtume wetu Muhammad-Swala na Salamu zimshukie- pamoja na kumtuhumu kwamba amefanya khiyana kwa kuacha kufikisha ujumbe ipasavyo, na hali ya kuwa Allaah anasema:

﴿يَا أَيُّهَا الرُّسُولُ بَلِّغْ مَا أُنْزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ وَإِنْ لَمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَغْتَ رِسَالَتَهُ وَاللَّهُ يَعْصِمُكَ مِنَ النَّاسِ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي الْقَوْمَ الْكَافِرِينَ﴾

“Fikisha ulioteremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi. Na ikiwa hukufanya hayo basi hukufikisha ujumbe wake. Na Allaah atakulinda na watu. Hakika Allaah hawaongozi watu makafiri”⁽²³⁾.

Pia Allaah anasema:

﴿الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتِمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا﴾

“Leo nimekukamilishieni Dini yenu, na nimekutimizieni neema yangu, na nimeridhia Uislamu kuwa ndio Dini yenu”⁽²⁴⁾.

Kwa hiyo Allaah ameridhia kwetu sisi Uislamu kuwa ndio dini yetu halafu kumbe maneno yake (Qur’an) imebadilishwa na kupotoshwa?!

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** Msiwafundishe wake zenu surat Yusuf, kwa sababu ndani yake kuna fitna, na wafundisheni surat An Nuur, kwa sababu ndani yake kuna mawaidha⁽²⁵⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Qur’an yote ni mawaidha, uongofu, na rehma kama alivyosema Allaah Subhaanahu Wata’alaa:

﴿يَا أَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَاءَكُمْ مَوْعِظَةٌ مِنْ رَبِّكُمْ وَشِفَاءٌ لِمَا فِي الصُّدُورِ وَهُدًى وَرَحْمَةٌ لِلْمُؤْمِنِينَ﴾

“Enyi watu, hakika yamekujieni mawaidha kutoka Mola wenu Mlezi, na pozo (la kuponyesha) yaliyomo vifuani, na Uwongofu na rehma kwa Waumini”⁽²⁶⁾.

²³-Surat Al Maida/

²⁴- Surat Al Maaida/3.

²⁵- Kitabu: [Al Furuu’ minal Kaafi] cha Al Kuleyn (Jz. 5, Uk. 516).

²⁶- Surat Yunus/57.

5- UIMAMU KWAO NI NGUZO NA HUMKUFURISH ASIYE AMINI HILO:

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** Haitimii imani kwa yule ambaye hawakubali Maimamu (wa Kishia)⁽²⁷⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Nguzo za Imani ni sita: 1- Kumuamini Allaah. 2- Malaika wake. 3- Vitabu vyake. 4- Mitume wake. 5- Kuamini siku ya mwisho (kiama), 6- Kuamini Qadar (utashi wa Allaah) kheri na shari (inatoka kwake). Wala haijakuja ndani ya Qur'an wala Hadithi kwamba Uimamu ni nguzo miongoni mwa nguzo za Imani.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Uimamu ni mwendelezo wa Utume, na dalili zilizokuja kuthibitisha kupelekwa Mitume na Manabii ndio hizohizo zinazo thibitisha kumuweka Imamu baada kufariki Mtume⁽²⁸⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Uimamu si mwendelezo wa Utume, lau ingelikuwa maneno hayo ni kweli Allaah angelibainisha hilo ndani ya Qur'an, kadhalika Mtume-Swala na Salamu zimshukie- angelitaja.

Allaah Ta'alaa anasema:

﴿الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتِمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا﴾

“Leo nimekukamilishieni Dini yenu, na nimekumizieni neema yangu, na nimeridhia Uislamu uwe ndiyo Dini”⁽²⁹⁾.

Amesema Imam Ibn Kathir-Allaah amrehemu:- “Hii ni miongoni mwa neema kubwa za Allaah juu ya umma huu, pale ambapo Allaah amewakamilishia wao Dini yao, hawahitaji Dini ya mwingine (asiyekuwa Allaah), wala Mtume mwingine asiyekuwa Mtume wao -Swala na Salamu zimshukie-,... wala hakuna halali isipokuwa ile aliyoihalalisha yeye (Mtume), wala haramu isipokuwa ile aliyoiharamisha Yeye, na wala hakuna (ruhusa ya kufanya jambo lolote) katika Dini isipokuwa alilofundisha Yeye...”⁽³⁰⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Makusudio ya Uimamu ni: Cheo cha Mungu, Allaah anamchagua (Imamu) kutokana na elimu yake iliyotangulia kwa waja wake, kama vile anavyomchagua Mtume,... tena huo Uimamu ni

²⁷- Kitabu: [‘Aqaaidul Al Imaamiyyah], cha Muhammad Ridwaa Mudhaffar (Uk. 78).

²⁸- Kitabu: [‘Aqaaidul Al Imaamiyyah], cha Muhammad Ridwaa Mudhaffar (Uk. 88).

²⁹- Surat Al Maaida/3.

³⁰- Kitabu: [Tafsiiru Ibn Kathir] (Jz. 5, Uk. 246).

msingi miongoni za misingi ya Dini ya Shia, haikamiliki Imani ya mtu yeyote isipokuwa kwa kuamini Uimamu]⁽³¹⁾.

- **Na sisi Ahluls Sunnah tunasema:** Haya ni maneno ya batili, Uimamu si cheo cha Mungu wala si msingi miongoni mwa misingi ya Dini, vipi Uimamu ni cheo cha Mungu hali ya kuwa Ally Bin Abi Twalib anasema:

"دَعُونِي وَالتَّمِسُوا غَيْرِي"

"Niacheni na mchagueni (mtu) mwingine"⁽³²⁾.

Pia amesema:

"وَإِنْ تَرَكْتُمُونِي فَأَنَا كَأَحَدِكُمْ وَلَعَلِّي أَسْمَعُكُمْ وَأَطُوعُكُمْ مَنْ وَلَيْتُمُوهُ أَمْرُكُمْ. وَأَنَا لَكُمْ وَزِيْرًا خَيْرٌ لَكُمْ مِنِّي أَمِيرًا"

"Na mkiacha kunichagua, basi mimi ni sawa mmoja wenu tu, na huenda mimi ndiye msikivu zaidi kwenu na mtiifu zaidi kwa yule mtakayemtawalisha jambo lenu (Amiri/Khalifa). Na kuwa mimi Waziri (msaidizi) ni bora kwenu kuliko kuwa Amiri"⁽³³⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanasema kwamba:** [Wamekubaliana Shia Imaamiyyah wote juu ya kwamba yeyote mwenye kukanusha Uimamu wa mmoja kati ya Maimamu kumi na mbili, na akapinga wajibu wa kumtii kama alivyofaradhisha Allaah huyo ni kafiri, mpotevu, na atastahiki kukaa motoni milele]⁽³⁴⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Hii ni dalili kwamba Shia Imaamiyyah wanawakufurisha Waislamu wote duniani, kwa sababu hakuna mwenye kuamini itikadi hii potofu isipokuwa Shia tu.
- **Shia Ithnaasharia wanasema kwamba:** [(sababu ya) kuitwa Washirikina au Makafiri wale wasio ukubali Uimamu wa Amiirul Muuminiin (Ally Bin Abi Twalib) na Maimamu (wengine) waliokuja baada

³¹- Kitabu: [Aslus Shiiat Wausuuluha] cha Muhammad Hussein Kaashiful Ghita (Uk. 102).

³²- Kitabu: [Nahjul Balaagha] (Jz. 1, Uk. 181). Kitabu hiki [Nahjul Balagha] kina Daraja kubwa mbele ya Shia Imaamiyyah. Anasema Sheikh wao Haadi Kaashiful Ghitwaa: "Mashia pamoja na kutafautiana makundi yao na mitazamo yao, wanaafikiana na kujisalimisha kwamba yote yaliyomo ndani ya kitabu Nahjul Balagha ni maneno ya Amiirul Muuminiin". Angalia: [Madaarikul Nahjil Balagha] (Uk. 190-191).

Bali Sheikh wao Ibn Abil Hadid wakatika anakisia kitabu hicho akasema: [Ni sawa na Qur'an tukufu].

³³- Kitabu: [Nahjul Balaagha] (Jz. 1, Uk. 182).

³⁴- Kitabu: [Haqqul yaqiin fiy ma'rifat Usuuli Ddiyn] cha Abdullah Shibbar (Jz. 2, Uk. 189).

yake katika kizazi chake, hiyo ni ishara kwamba watu hao ni wenye kukaa motoni milele]⁽³⁵⁾.

- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Uimamu si katika mambo ya misingi ya Dini ambayo anakuwa kafiri yule mwenye kupinga, na kumpa hukumu ya ukafiri atakayepinga itikiadi hiyo, bali huko ni kuwakufurisha Waislamu wote duniani bila ya hatia, kwa sababu hakuna anayeamini Uimamu kuwa ni nguzo isipokuwa Shia Imaamiyyah Ithnaasharia.

6- KUMKOSEA ADABU MTUME صلى الله عليه وسلم BINT ZAKE NA AHLUL BAYT WOTE:

- **Shia Ithnaasharia wanasema kwamba:** [Mtume -Swala na Salamu zimshukie- wakati alipozaliwa, alikosa maziwa (ya kunyonya) katika baadhi ya masiku, Abu Twalib akamuweka kwenye titi lake na Allaah akateremsha ndani ya titi hilo maziwa, akamnyonyesha kwa masiku kadhaa, mpaka alipompata (mjakazi) Halima As Sa'diyyah, akampatia (amnyonyeshe)]⁽³⁶⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Kisa hiki ni uwongo uliotungwa, unapingana na Akili, Sheria na Ada, na ndani yake kuna kumkosea adabu Mtume-Swala na Salamu zimshukie- kadhaalika Ally Bin Abi Twalib, kwa sababu wamemsifu baba yake kuwa alikuwa na matiti na yanatoa maziwa].
- **Shia Ithnaasharia wanasema kwamba:** [Ally ni shujaa zaidi kuliko Mtume-Swala na Salamu zimshukie-, bali yeye Mtume-Swala na Salamu zimshukie- hakupewa ushujaa kabisa]⁽³⁷⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Mtume-Swala na Salamu zimshukie- ni shujaa zaidi kuliko mtu yeyote, amesema Ally wakati akielezea ushujaa wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- amesema: **“Tulikuwa pindi vita vinapokuwa vikali na watu wanapokutana na maadui, tunataka kinga kwa Mtume -Swala na Salamu zimshukie-, hakuna juu yetu aliye shujaa mkubwa zaidi kwa maadui kuliko yeye (Mtume)”**⁽³⁸⁾.

³⁵- Kitabu: [Bihaarul Anwaa: Jz. 23 Uk. 390].

³⁶- Kitabu: [Usuulul Kaafi] cha Al Kulain (Jz. 1, Uk. 447).

³⁷- Kitabu: [Al Anwaaru Nnu'maniyyah] cha Ni'matullah Al Jazaaair (Jz. 1, Uk. 17).

³⁸- Kitabu: [Ahmad 1346]. Na **“Sanadi yake ni sahihi”**. Kwa uhakiki wa Sheikh Ahmad Shakir katika Musnad:

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Mtume-Swala na Salamu zimshukie- alikuwa halali mpaka abusu uso wa Fatma au baina ya matiti yake]⁽³⁹⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Huu ni utovu wa nidhamu kwa Mtume -Swala na Salamu zimshukie-, haiwezekani kupatikana kitendo hicho kwa Mtume wa Allaah!
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Mtume-Swala na Salamu zimshukie- hana mtoto wa kike isipokuwa Fatma tu, ama Ruqayyah, Ummu Kulthum na Zainab hao ni watoto wake wa kuwalea tu]⁽⁴⁰⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Zainab, Ruqayyah, Ummu Kulthum na Fatma, wote hao ni watoto wake Mtume-Swala na Salamu zimshukie- (kwa makubaliano ya Maulamaa wa Sira), na watoto wote amezaa na mke wake Bibi Khadija, na watoto wake wa kiume ni Qassim na Abdullaah, ambao pia amezaa na Bibi Khadija, ama Ibrahim amezaa na mkewe anayeitwa Maria⁽⁴¹⁾.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakika Hassan Bin Ally ndiye aliye wadhalilisha waumini (Mashia), kwa sababu yeye alimpa Bai'a (kiapo cha utiifu) Mu'awiya Ibn Abi Sufyan]⁽⁴²⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Hassan Bin Ally -Allaah amridhie- alijiuzulu Ukhalifa na kumuachia Mu'awiya kwa ajili ya pupa ya kuwaunganisha Waislamu na kulifanya neno lao liwe moja, mpaka ukaitwa mwaka huo kuwa ni mwaka wa Umoja, na hapo ilitimia ile kauli ya Mtume -Swala na Salamu zimshukie- aliposema: **"Hakika mtoto wangu huyu (Hassan) ni Sayyid (bwana mkubwa), na Allaah atapatanisha kupitia yeye baina ya makundi mawili ya Waislamu"**⁽⁴³⁾.

Hii ni daraja na sifa kubwa kwa Hassan -Allaah amridhie-, ameachia madaraka si kwa unyonge wala udhaifu hapana, bali ni kutaka yaliyo mbele ya Allaah, na kuzilinda damu za Waislamu, akatanguliza maslahi ya umma.

³⁹- Kitabu: [Bihaaru al Anwaar] cha Al Majlis: (Jz. 42, Uk. 43).

⁴⁰- Kitabu: [Daairutul Ma'arifil Islaamiyyah Sshi'yyah] (Jz. 1, Uk. 27).

⁴¹- Kitabu: [Al Ma'arif] cha Ibn Qutaiba (Uk. 132-133)

⁴²- Kitabu: [Rijaalu al-Kisshi] (Uk. 103).

⁴³- Kitabu: [Bukhari] (2704).

7- KUWAKUFURISHA KWAO MAMA WA WAUMINI AISHA NA HAFSWA

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Inawezekana kwa mke wa Mtume akawa kafiri, kama vile mke wa (Nabii) Nuh na Lut. Na makusudio ya mke wa Mtume hapo ni Aisha-Allaah amridhie-]⁽⁴⁴⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Maneno haya yanapingwa na Qur'an tukufu, kwa kauli yake Allaah Ta'alaa:

﴿وَلَا تُمَسِّكُوا بِعَصَمِ الْكَوَافِرِ﴾

“Wala msiwaoe wanawake makafiri”⁽⁴⁵⁾.

Kwa hiyo haiwezekani Mtume kukaa na mke kafiri, kwa sababu yeye ndio wa mwanzo kufanyia kazi maelekezo yaliyo ndani ya Qur'an.

Na Allaah amewaita wakeze Mtume kuwa ni mama wa Waumini, vipi wawe ni makafiri au washirikina?! Allaah anasema:

﴿الَّتِي أُولَىٰ بِالْمُؤْمِنِينَ مِنْ أَنْفُسِهِمْ وَأَزْوَاجُهُ أُمَّهَاتُهُمْ﴾

“Nabii ni bora zaidi kwa Waumini kuliko nafsi zao, na wake zake ni mama zao”⁽⁴⁶⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** Aisha ameritadi (ametoka katika Uislamu) baada ya kufariki Mtume-Swala na Salamu zimshukie-, kama lilivyoritadi kundi kubwa la Maswahaba⁽⁴⁷⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Kauli hii inapingana na Qur'an, kwa sababu Allaah amemtakasa Aisha, na akateremsha Aya zenye kubainisha wazi jambo hili, na watu wanazisoma mpaka siku ya kiama, na Waislamu katika Maswahaba na Ahlul Bayt bado waliendelea kumuuliza Aisha mambo mbalimbali ya dini na hukumu zake mpaka Allaah alipomfisha.
- **Shia Ithnaasharia wanasema kwamba:** [Aisha amekusanya dinari Elfu arobaini za uzinifu na akazigawanya kwa watu wenye kumchukia Ally!]⁽⁴⁸⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Kumtukana Aisha ni sawa na kumtukana yule aliyemchagua yeye kuwa mke wake, ikiwa mama wa

⁴⁴- Kitabu: [Hadiithul Ifki] cha Ja'far Murtadhwa (Uk. 17).

⁴⁵- Surat Al-Mumtahina/10.

⁴⁶-Surat Al-Ahzaab/6.

⁴⁷- Kitabu: [As Shihaabu Tthaaqib] cha Yusuf al-Bahraani (Uk. 236).

⁴⁸- Kitabu: [Mashaariqu Anwaaril Yaqiin] cha Rajab Al-Barsi (Uk. 86).

Waumini wametukanwa kiasi hiki na Mashia, basi vipi watafaa kuwa wake wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie- ambaye alikuwa ni msafi na mtwahaifu kuliko watu wote!, kama Allaah alivyosema:

﴿الْحَيْثُ لِلْخَيْثِ وَالْخَيْثُ لِلْخَيْثِ وَالْطَّيِّبُ لِلطَّيِّبِ وَالطَّيِّبُ لِلطَّيِّبِ أُولَئِكَ مُبَرَّءُونَ مِمَّا يَقُولُونَ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ﴾

“Wanawake waovu ni wa wanaume waovu, na wanaume waovu ni wa wanawake waovu. Na wanawake wema ni wa wanaume wema na wanaume wema ni wa wanawake wema. Hao wameepushwa na hayo wanayoyasema, wao watapata msamaha na riziki ya ukarimu”⁽⁴⁹⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Aisha alifanya uzinifu, na kauli yake aliposema: (hao wameepushwa na hayo wanayoyasema), anakusudia kumkanushia Mtume wake uzinifu wala si yeye (Aisha)]⁽⁵⁰⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Allaah amemsafisha Aisha na Aya mbalimbali kutoka mbinguni na kuepusha na tuhuma hizo zilizoletwa na wanafiki, na Aya hizo zinasomwa mpaka siku ya kiamaa.

Allaah anasema:

﴿إِنَّ الَّذِينَ جَاءُوا بِالْإِفْكِ عُصْبَةٌ مِّنْكُمْ لَا تَحْسَبُوهُ شَرًّا لَّكُم بَلْ هُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ لِكُلِّ امْرِئٍ مِّنْهُمْ مَا أَكْتَسَبَ مِنَ الْإِثْمِ وَالَّذِي تَوَلَّى كِبْرَهُ مِنْهُمْ لَهُ عَذَابٌ عَظِيمٌ﴾

“Hakika wale walioleta uwongo ni kundi miongoni mwenu. Msifikiri ni shari kwenu, bali ni kheri kwenu. Kila mtu katika wao atapata aliyoyachuma katika madhambi. Na yule aliyejitwika sehemu yake kubwa (katika uzushi huo) miongoni mwao, atapata adhabu kubwa”⁽⁵¹⁾.

Yeyote mwenye kumtuhuma mama wa Waumini Aisha-Allaah amridhie-baada ya ushahidi huu wa Allaah kutoka mbinguni, huyo anamtuhumu Allaah ‘Azza Wajalla, kadhaalika anakituhumu Kitabu chake Qur’an tukufu.

⁴⁹- Surat An nuur/26.

⁵⁰- Kitabu: [As swiraatul Mustaqim] cha Zainu Ddiin An nabaatwi (Jz. 3, Uk. 165).

⁵¹- Surat An Nuur/11.

- **Shia Ithnaasharia wanasema kwamba:** [Hafswa amekufuru pale aliposema:

﴿مَنْ أَنبَأَكَ هَذَا﴾

“Nani aliyekwambia haya?”⁽⁵²⁾.

Kisha Allaah akasema kuhusu yeye Hafsa na Aisha:

﴿إِنْ تَوْبًا إِلَى اللَّهِ فَقَدْ صَغَتْ قُلُوبُكُمَا﴾

“Mkiwa nyinyi wawili hamkutubia basi nyoyo zenu zimekwisha pondokea huko”.

(wamesema): neno (Zaigh: الزَّيْغُ) ni ukafiri. Aisha na Hafswa wameafikiana juu ya kumnwyesha sumu Mtume-Swala na Salamu zimshukie- na Allaah alipomjulisha Mtume wake kitendo chao hicho alitaka kuwaua, wakaapa kwamba wao hawajafanya kabisa jambo hilo, baada ya hapo Allaah akateremsha aya:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ كَفَرُوا لَا تَعْتَذِرُوا الْيَوْمَ إِنَّمَا تُجْرُونَ مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ﴾

“Enyi mliokufuru, msilete udhuru leo. Hakika mtalipwa mliyokuwa mkiyatenda”^{(53) (54)}.

- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Maneno haya ni batili, maana ya neno Zaigh ni kumili upande na kwenda kombo, na mke mmoja kumlilia wivu mke mwenzie ni jambo la kimaumbile, wala hilo halimtoi katika Uislamu na kumfanya kuwa kafiri kama wanavyodai Mashia.

8- KUVUKA KWAU MIPAKA KUHUSU ALLY -ALLAAH AMRIDHIE-

- **Shia Ithnaasharia wanasema kwamba:** [Allaah siku ya Miraji alimsemesha Mtume wake kwa sauti ya Ally Bin Abi Twalib na lugha yake]⁽⁵⁵⁾.

⁵²- Surat At Tahrim/3.

⁵³- Surat At Tahrim/4.

⁵⁴- Kitabu: [As Swiraatul Mustaqim] cha Zainu Ddiin An Nabaatwi (Jz. 3, Uk. 168).

⁵⁵- Kitabu: [Kashful yaqin fiy Fadhwaail Amiril Muuminiin] cha Hassan Bin Yusuf Al Hilly (Uk. 229).

- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Huku ni kuvuka mipaka juu ya Ally-Allaah amridhie-, Allaah amejisifu nafsi yake kwamba hakuna kitu chochote ni mfano wake yeye, akasema:

﴿لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ﴾

“Hakuna kitu chochote ni mfano wake. Na yeye ni mwenye kusikia Mwenye kuona”⁽⁵⁶⁾.

Na Ahlus Sunnah wote wamekubaliana juu ya kwamba yeyote mwenye kumfananisha Allaah ana viumbe vyake amekufuru, na Allaah ametakasika na hilo.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Ally Bin Abi Twalib ndiye mwenye kugawa pepo na moto, atawaingiza watu wa peponi katika pepo na watu wa motoni katika moto⁽⁵⁷⁾.

- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Pepo na moto vipo katika mamlaka ya Allaah, allaah atamuingiza peponi yule amtakaye kwa fadhila zake, hali ya kuwahurumia watu wema, na atamuingiza motoni yule amtakaye kwa hekima yake, hali ya kuwa ni adhabu kwa watu waovu. Allaah anasema:

﴿يُعَذِّبُ مَنْ يَشَاءُ وَيَرْحَمُ مَنْ يَشَاءُ وَإِلَيْهِ تُقْلَبُونَ﴾

“Humuadhibu amtakaye na humrehemu amtakaye. Na kwake Yeye tu mtarejeshwa”⁽⁵⁸⁾.

Na Ally Bin Abi Twalib ni miongoni mwa waja wake, wala hamiliki yeye pepo wala moto.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Allaah atamuingiza peponi mwenye kumtii Ally hata kama atamuasi Allaah Ta’alaa, na atamuingiza motoni mwenye kumuasi Ally hata kama atamtii Allaah Ta’alaa]⁽⁵⁹⁾.

- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Kumtii Allaah na Mtume-Swala na Salamu zimshukie- kunatangulizwa juu ya kila kitu, kwa hiyo mwenye kumtii Allaah na Mtume wake huyo ameokoka na adhabu ya Allaah, na mwenye kumuasi Allaah na Mtume wake ameangamia na kupata hasara.

⁵⁶- Surat As Shuura/11.

⁵⁷- Kitabu: [Baswaairu Ddarajaat] cha As Swaffaar (Jz. 8, Uk. 235).

⁵⁸- Surat Al’Ankabut/21.

⁵⁹- Kitabu: [Kashful yaqiin Fii Fadhwaaaili Amiriil-Mu’miniin] cha Hasan Bin Yusuf Al Hilly (Uk. 8).

Allaah anasema:

﴿قُلْ أَطِيعُوا اللَّهَ وَالرَّسُولَ فَإِنْ تَوَلَّوْا فَإِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ الْكَافِرِينَ﴾

“Sema: Mtiini Allaah na Mtume. Na mkikengeuka basi Allaah hawapendi makafiri”⁽⁶⁰⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Ally ni siri ya Allaah kwa Mitume, na kwamba Allaah aliposema: Ewe Muhammad, nimempeleka Ally akiwa pamoja na Manabii wengine kwa siri (Ally alikuwepo kila zama lakini alikuwa haonekani), na kwako nimempeleka kwa dhahiri (anaonekana)]⁽⁶¹⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Hakuna mahali popote ndani ya Qur’an wala Sunnah alipotajwa (Ally) kuwa ni Wasii wa Manabii, isipokuwa Mashia wanakusudia kumpa Ally cheo cha juu kuliko Mitume wa Allaah.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Ally ni alama ya Muhammad na kwamba Muhammad analingania kwenye Ukhalifa wa Ally]⁽⁶²⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Alama ya Mtume-Swala na Salamu zimshukie- ni Qur’an wala si Ally-Allaah amridhie-, Allaah amewapoteza washirikina wa Kikureishi kwa Qur’an wala si kwa sababu ya kumuasi Ally. Allah amewatuma Mitume kwenda kulingania Tauhid, wala hakuwapeleka kwenda kulingania Ukhalifa wa Ally, Allaah anasema:

﴿وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا نُوحِيَ إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ﴾

“Na hatukumtuma kabla yako Mtume wowote ila tulimfunulia wahyi ya kwamba hapana Muabudiwa (wa haki) isipokuwa mimi tu. Basi niabuduni”⁽⁶³⁾.

Kadhaalika Allaah anasema:

﴿وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنْ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ﴾

“Na hakika katika kila umma tulipeleka Mtume, (akawa anawaambia) ya kwamba: Muabuduni Allaah na jiepusheni na Twaghut”⁽⁶⁴⁾⁽⁶⁵⁾.

⁶⁰- Surat Aal Imraan/32.

⁶¹- Kitabu: [Al Asraarul ‘Alawiyyah] cha Muhammad Al Mas’oudiy (Uk. 181).

⁶²- Kitabu: [Baswaairu Ddarajaat] cha Muhammad Swaffaar (Uk. 91).

⁶³- Surat Al-Anbiyaa/25.

⁶⁴- Twaghut ni kila anayeabudiwa kinyume na Allaah, sawa ni mtu, mti, pango n.k

⁶⁵- Surat An Nahli/36.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Dini haikamiliki isipokuwa kwa kuutangaza Ukhalifa wa Amiril Muuminina Ally Bin Abi Twalib]⁽⁶⁶⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Allaah ameikamilisha Dini hii bila kutangazwa U khalifa wa Ally-Allaah amridhie-.
Allaah anasema:

﴿الْيَوْمَ اكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتِمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا﴾

“Leo nimekukamilishieni Dini yenu, na nimekutimizieni neema zangu, na nimeridhia Uislamu uwe ndio Dini”⁽⁶⁷⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Ally ataingia peponi kabla ya Mtume Muhammad-Swala na Salamu zimshukie-]⁽⁶⁸⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Huu ni miongoni mwa uongo wa Mashia, Mtume -Swala na Salamu zimshukie- siku ya kiamaa ataenda kwenye mlango ya pepo aombe kufunguliwa, na baada ya kujitambulisha Malaika atamwambia:

"بِكَ أَمَرْتُ لَا أَفْتَحُ لِأَحَدٍ قَبْلَكَ"

“Kwa ajili yako tu nimeamrisha, wala simfungulii yeyote kabla yako”⁽⁶⁹⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Sauti ya radi ni amri ya Swahibu wenu, wakasema: Ni nani huyo Swahibu wetu? Wakasema: Huyo ni Amiril Mu’miniina Ally Bin Abi Twalib]⁽⁷⁰⁾.
- **Na sisi Ahlis Sunnah tunasema:** Huku ni kumkosea adabu Allaah Subhaanah, umeme wa radi (umweko/umwesa) na mvua, vyote hivyo hutokea kwa amri ya Allaah bila kushirikiana na yeyote katika viumbe wake, kwa sababu hayo ni katika utendaji kazi unaomhusu yeye pakee (Tauhid Rrubuubiyah), Allaah Ta’alaa amesema:

⁶⁶- Kitabu: [Al-ihitjaaj] cha At Twabarsi (Jz. 1, Uk. 57).

⁶⁷- Surat Al-Maida/3.

⁶⁸- Kitabu: [‘Ilalus Sharaal’] Cha Ibn Baabawaih Al Qummi (Uk. 205).

⁶⁹- Kitabu: [Sahihi Muslim] (333).

⁷⁰- Kitabu: [Al Ikhtiswaas] cha Al Mufid (Uk. 327).

﴿وَمِنْ آيَاتِهِ يُرِيكُمْ الْبَرْقَ خَوْفًا وَطَمَعًا وَيُنْزِلُ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَيُخْرِجُ بِهِ الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ﴾

“Na miongoni mwa ishara zake anakuonyesheni umeme (wa radi) kwa ajili ya kukutieni khofu na tamaa. Na anakuteremshieni maji kutoka mbinguni, na kwa hayo huifufua ardhi baada ya kufa kwake, hakika katika hayo zipo ishara kwa watu wanaozingatia”⁽⁷¹⁾.

Pia Allaah anasema:

﴿هُوَ الَّذِي يُرِيكُمْ الْبَرْقَ خَوْفًا وَطَمَعًا وَيُنْشِئُ السَّحَابَ الثِّقَالَ ** وَيُسَبِّحُ الرَّعْدُ بِحَمْدِهِ وَالْمَلَائِكَةُ مِنْ خِيفَتِهِ وَيُرْسِلُ الصَّوَاعِقَ فَيُصِيبُ بِهَا مَنْ يَشَاءُ وَهُمْ يُجَادِلُونَ فِي اللَّهِ وَهُوَ شَدِيدُ الْمِحَالِ﴾

“Yeye ndiye anaye kuonyesheni umeme (wa radi) kwa khofu na tamaa, na huyaleta mawingu mazito ** Na radi inamtakasa Allaah pamoja na kumhimidi, na Malaika, kwa kumkhofu yeye. Naye hupeleka mapigo ya radi yakampata amtakaye, nao wanabishana juu ya Allaah, naye ni mwenye adhabu kali”⁽⁷²⁾.

➤ **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakika Ally Bin Abi Twalib anahuisha wafu na huleta faraja kwa waliosibiwa na majanga]⁽⁷³⁾.

▪ **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Jambo la kufufua maiti ni amri ya Allaah Subhaanah, wala hakuna mtu yeyote aliyepewa muujiza huu isipokuwa Nabii wa Allaah Issa-alaihis swalaatu was salaam- kwa idhini yake Allaah Ta’alaa, Allaah anasema:

﴿وَأُخِي الْمَوْتَى بِإِذْنِ اللَّهِ﴾

“Na ninawafufua maiti kwa idhini ya Allaah”⁽⁷⁴⁾.

➤ **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Kuna mbwa aliwauma Maswahaba wawili kwa ajili ya kulipa kisasi kwa Ally Bin Abi Twalib, baada ya kumpanda yeye mori wa kiarabu, na (mara mmoja) punda aliwahi kutoa ushahidi kwamba Ally ni Walii wa Allaah na Wasii wa Mtume wake]⁽⁷⁵⁾.

⁷¹- Surat Ar Ruum/24.

⁷²- Surat Ar Ra’d/12-13.

⁷³- Kitabu: [‘uyuunul Mu’jizaat] cha Hussein Abdul Wahaab (150).

⁷⁴- Surat Aal Imraan/49.

⁷⁵- Kitabu: [Bihaarul Anwaar] (Jz. 17, Uk. 306) na (Jz. 41, Uk. 247).

9- KUVUKA KWAO MIPAKA KUHUSU FATMA

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Fatma, Hassan na Hussein na kizazi chote cha Hussein ni Ma'sum (wamekingwa na kutenda madhambi), kinyume na kizazi cha Hassan (wao si Ma'sum)]⁽⁷⁶⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Hakuna dalili yoyote ndani ya Qur'an wala Sunnah juu ya kwamba watu hao (waliotajwa) wamekingwa na kutenda madhambi, kwa sababu wamekubaliana maulamaa wote kwamba jambo la kuingwa na kutenda madhambi linapatikana kwa Manabii tu, ama watu wengine waliobaki inawezekana kwao kufanya madhambi makubwa au madogo, na hao (Fatma, Hassan na Hussein) si Mitume wala si Manabii.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** (Allaah anasema): [Lau si Ally asingeumbwa Muhammad, na lau si Fatma msingeumbwa nyinyi (Mtume Muhammad na Ally)]⁽⁷⁷⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Ally, Fatma na watu wote wakiwemo Manabii, wote hao hawajaumbwa isipokuwa kwa ajili ya kumuabudu Allaah peke yake, Allaah anasema:

﴿وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ﴾

“Na sijawaumba majini na watu ila waniabudu”⁽⁷⁸⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Fatma ni umbile la Mungu lenye nguvu limedhihiri katika kiwiliwili cha mwanamke]⁽⁷⁹⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Huku ni kuvuka kwao mipaka kuhusu Fatma-Allaah amridhie-, Fatma yeye ni mtu sawa na watu wengine, na Mtume-Swala na Salamu zimshukie- alisema kumwambia Fatma:

«وَيَا فَاطِمَةُ بِنْتُ مُحَمَّدٍ سَلِّينِي مَا شِئْتُ مِنْ مَالٍ لَا أُغْنِي عَنْكَ مِنَ اللَّهِ شَيْئًا»

⁷⁶- Kitabu: [‘Aqaaidul Imaamiyyah] cha Ridhwa Mudhwaffar (Uk. 89 na 98).

⁷⁷- Kitabu: [Al Asraarul Faatwimiyyah] cha Muhammad Al Masoudiy (Uk. 98).

⁷⁸- Surat Ad Dhaariya/56.

⁷⁹- Kitabu: [Al Asraarul Faatwimiyyah] cha Muhammad Al Masoudiy (Uk. 355).

“Ewe Fatma Bint Muhammad, niombe katika mali yangu unachotaka, lakini sitokunufaisha wewe mbele ya Allaah kwa chochote”⁽⁸⁰⁾.

Ahlus Sunnah wamehifadhi fadhila za Fatma-Allaah amridhie- ndani ya vitabu vyao, kama ilivyokuja katika hadithi aliyoipokea Aisha -Allaah amridhie-, (hii ni alama kwamba Aisha alikuwa anampenda Fatma) na kwamba alimsikia Mtume-Swala na Salamu zimshukie- anasema:

«أَفْضَلُ نِسَاءِ الْجَنَّةِ أَرْبَعٌ: مَرْيَمُ بِنْتُ عِمْرَانَ، وَخَدِيجَةُ بِنْتُ خُوَيْلِدٍ، وَفَاطِمَةُ ابْنَةُ مُحَمَّدٍ، وَأَسِيَّةُ ابْنَةُ مُزَاحِمٍ»

“Wanawake bora wa peponi ni wanne: Maryam Bint Imran, Khadija Bint Khuwailid, Fatma Bint wa Muhammad -Swala na Salamu zimshukie-, na Asia Bint Muzaahim”⁽⁸¹⁾.

Hii ni alama kwamba Aisha-Allaah amridhie- alikuwa anampenda Fatma-Allaah amridhie- na kuvunja madai ya Shia Imaamiyyah na uwongo wao juu ya Aisha-Allaah amridhie.

- **Shia Ithnaasharia wanaitakidi kwamba:** [Fatma alikuwa anamsemesha mama yake hali ya kuwa yupo tumboni (mimba)]⁽⁸²⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Kauli hii haina dalili yoyote yenye kutegemewa, bali kauli yao hii ni ushahidi kwamba wao wanawatukuza zaidi Maimamu wao kuliko Manabii wa Allaah-Alahimus Salaam-, kwa sababu Manabii ambao ni watu bora kuliko viumbe wote, haijathibiti kwamba lilitokea kwao mfano wa jambo hili, vipi kwa mtu mwingine aliye chini kwa daraja kuliko wao?!
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Mwenye kutukanusha sisi (maimamu) ni sawa na aliyemkanusha Allaah na huyo yupo katika hukumu ya mshirikina]⁽⁸³⁾.
- **Na sisi Ahlius Sunnah tunasema:** Yeyote ambaye kauli yake itapingana na kauli ya Allaah au Mtume-Swala na Salamu zimshukie- basi kauli yake itarudishwa na kupingwa.

⁸⁰- Kitabu: [Bukhari] (2753) na [Muslim] (351).

⁸¹- Kitabu: [Musnad Ahmad] (2957).

⁸²- Kitabu: [Faatimat Az zahraa minal Mahdi Ilal Lahdi] cha Muhammada Qaz-wiini (Uk. 38).

⁸³- Kitabu: [Usuulul Kaafi] cha Al Kuleyn (Jz. 1, Uk. 67).

Amesema Imam Malik-Allaah amrehemu:-

"كُلُّ أَحَدٍ يُؤْخَذُ مِنْ قَوْلِهِ وَيُتْرَكُ، إِلَّا صَاحِبَ هَذَا الْقَبْرِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ"

"Kila mtu huchukuliwa kauli na kukataliwa, isipokuwa mwenye kaburi hili -Swala na Salamu zimshukie-"⁽⁸⁴⁾.

➤ **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Maimamu kumi na mbili wa Kishia ni bora kuliko Mitume na Manabii]⁽⁸⁵⁾.

▪ **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Jambo hili ni kinyume na itikadi ya Waislamu wote, kwa sababu itikadi ya Waislamu duniani ni kwamba Manabii na Mitume ndio watu bora, hasa wale Ulul 'Azmi.

Allaah anasema:

﴿إِنَّ اللَّهَ أَصْطَفَىٰ آدَمَ وَنُوحًا وَآلَ إِبْرَاهِيمَ وَآلَ عِمْرَانَ عَلَى الْعَالَمِينَ﴾

"Hakika Allaah alimteua Adam, Nuh, Ukoo wa Ibrahim, na Ukoo wa Imran juu ya walimwengu wote"⁽⁸⁶⁾.

Na pia anasema:

﴿تِلْكَ الرُّسُلُ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ مِنْهُمْ مَنْ كَلَّمَ اللَّهُ وَرَفَعَ بَعْضَهُمْ دَرَجَاتٍ وَآتَيْنَا عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ الْبَيِّنَاتِ وَأَيَّدْنَاهُ بِرُوحِ الْقُدُسِ﴾

"Mitume hao tumewatukuza baadhi yao juu ya baadhi nyingine. Katika hao wapo ambao Allaah alisema nao, na wengine akawapandisha vyeo. Na tulimpa Isa mwana wa Maryam hoja zilizo waziwazi, na tukamtia nguvu kwa Roho Takatifu"⁽⁸⁷⁾.

➤ **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Maimamu wa Kishia wanayajua yaliyopita yanayokuja, na kwamba hakifichiki kwao kitu chochote, na wao hawafi isipokuwa kwa hiyari yao]⁽⁸⁸⁾.

▪ **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Hakuna anayejua ghaibu (mambo yaliyofichikana) isipokuwa Allaah:

⁸⁴- Kitabu: [Siyar a'laami Nnubalaa] (Jz. 1, Uk. 55).

⁸⁵- Kitabu: [Al Anwaaru Nnu'maaniyyah] cha Ni'matullaahi Al Jazaairiy (Jz. 3, Uk. 308).

⁸⁶- Surat Aal 'Imraan/33.

⁸⁷- Surat Al-Baqara/253.

⁸⁸- Kitabu: [Usuulul Kaafi] (Jz. 1, Uk. 258-260).

﴿وَعِنْدَهُ مَفَاتِيحُ الْغَيْبِ لَا يَعْلَمُهَا إِلَّا هُوَ وَيَعْلَمُ مَا فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ وَمَا تَسْقُطُ مِنْ وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٌ فِي ظُلْمَةٍ الْأَرْضِ وَلَا رَطْبٌ وَلَا يَأْسٌ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُبِينٍ﴾

“Na ziko kwake yeye tu funguo za ghaibu hakuna azijuaye ila Yeye tu. Na Yeye anajua kilioko nchi kavu na baharini. Na halidondoki jani lolote ila analijua. Wala punje yoyote katika giza la ardhi, wala kinyevu, wala kikavu ila kimo kwenye kitabu chenye kinachobainisha”⁽⁸⁹⁾.

Na Mtume-Swala na Salamu zimshukie- pamoja na kwamba Yeye ni mbora wa viumbe wote lakini Allaah Ta’alaa amemuamrisha aseme:

﴿قُلْ لَا أَمْلِكُ لِنَفْسِي نَفْعًا وَلَا ضَرًّا إِلَّا مَا شَاءَ اللَّهُ وَلَوْ كُنْتُ أَعْلَمُ الْغَيْبِ لَاسْتَكْنَرْتُ مِنَ الْخَيْرِ وَمَا مَسَّنِيَ السُّوءُ إِنْ أَنَا إِلَّا نَذِيرٌ وَبَشِيرٌ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ﴾

“Sema: Siimilikii nafsi yangu manufaa wala madhara, ila apendavyo Allaah. na lau kuwa ninayajua ya ghaibu ningejizidishia mema mengi, wala lisinge nigusa ovu lolote. Mimi si chochote ila ni mwonyaji na mbashiri kwa watu wanao amini”⁽⁹⁰⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** kwamba Imam ana cheo cha kuhimidiwa (Maqaamam Mahmuuda), na wanazo daraja za juu, na utawala wa ulimwengu ni wao, viumbe wote duniani wananyenyekea kwao⁽⁹¹⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Haya ni matusi na kejeli za wazi kwa Mitume na Manabii wa Allaah akiwemo Mtume wetu Muhammad-Swala na Salamu zimshukie-, kwa sababu wamewafanya Maimamu wa Ahlul Bayt wana daraja na cheo cha juu zaidi kuliko Mitume wote wa Allaah.
- **Na Shia Ithanaasharia wanasema:** [Maimamu kumi na mbili wa shia wanayo mamlaka katika ulimwengu huu tafauti na mamlaka ya Allaah, na mamlaka hayo ni sawa na mamlaka ya Allaah Ta’alaa juu ya viumbe]⁽⁹²⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Katika utawala wa Allaah juu ya viumbe hakuna yeyote anayeshirikiana naye, si Malaika aliyekurubishwa kwa Allaah wala Mtume aliyetumwa na Allaah.

⁸⁹- Surat Al-An’aam/59.

⁹⁰- Surat Al-A’raaf/188.

⁹¹- Kitabu: [Tahriirul Wasiilah] cha Al-Khomein (Uk. 52).

⁹²- Kitabu: [Misbaahul Fuqaaha] cha Ibnul Qassim Al-Khu’ayy (Jz. 5, Uk. 33).

Allaah anasema:

﴿قُلْ مَنْ يَرْزُقُكُمْ مِنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ أَمَّنْ يَمْلِكُ السَّمْعَ وَالْأَبْصَرَ وَمَنْ يُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَيِّتِ وَيُخْرِجُ الْمَيِّتَ مِنَ الْحَيِّ وَمَنْ يُدِيرُ الْأَمْرَ فَسَيَقُولُونَ اللَّهُ فَقُلْ أَفَلَا تَتَّقُونَ﴾

“Sema: Ni nani anayekuruzukuni kutoka mbinguni na ardhini. Au ni nani anayemiliki kusikia na kuona. Na nani amtoaye hai kutoka maiti, na akatoa maiti kutoka aliye hai. Na nani anaye yaendesha mambo yote? Watasema: Allaah. Basi sema: kwanini Hamumchi?”⁽⁹³⁾.

➤ **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakuna kizuizi chochcote cha kuwazuia Maimamu wa Kishia kupitisha mambo (ya ulimwengu) kwa idhini yao, na kuipitisha usiku wa Laylatul Qadri n.k...] ⁽⁹⁴⁾.

▪ **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Mambo haya yote anahusika nayo Allaah pekee pasi na kumshirikisha yeyote katika viumbe, na kuhusu Laylatul Qadri. Allaah anasema:

﴿تَنْزِيلُ الْمَلَائِكَةِ وَالرُّوحِ فِيهَا بِإِذْنِ رَبِّهِمْ مِّنْ كُلِّ أَمْرٍ﴾

“Wanashuka Malaika na Roho (Jibril) katika usiku huo kwa idhini ya Mola wao kwa ajili ya kila jambo jema”. [Surat Al Qadr/4].

Wala Allaah hakusema kwa idhini ya Maimamu kumi na mbili.

➤ **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hussein alikuwa ananyonya kwenye kidole gumba cha Mtume -Swala na Salamu zimshukie- kiasi cha kumtosheleza kwa siku mbili au tatu] ⁽⁹⁵⁾.

▪ **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Hakuna riwaya sahihi yenye kutegemewa inayothibitisha jambo hilo, wala Mtume-Swala na Salamu zimshukie- hahitaji kuzuliwa uwongo ili kuthibitisha miujiza yake.

➤ **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Maimamu kumi na mbili wa Shia mimba zao hubebwa mbavuni (si matumboni) na wakati wa kuzaliwa kwao hutokea kwenye mapaja, wala huwagusi wao uchafu (damu na nifasi)] ⁽⁹⁶⁾.

▪ **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Ikiwa kubebwa mimba tumboni na kuzaliwa kutoka katika fuko la uzazi ni uchafu, watasema nini Shia kuhusu

⁹³- Surat Yunus/31.

⁹⁴- Kitabu: [Al Burhaanul Qaatwi'] cha Muhammad Taqiy Al Bahjat (Uk. 14).

⁹⁵- Kitabu: [Usuulu al Kaafi] cha Al Kuleyn (Jz. 1, Uk. 465).

⁹⁶- Kitabu: [Madiinatul Ma'ajiz] cha Hashim Al Bahraani (Jz. 8, Uk. 22).

mimba ya Mtume -Swala na Salamu zimshukie- ambayo ilibebwa na mama Amina tumboni na kuzaliwa kutoka kwenye fuko la uzazi?!

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakika Allaah, Malaika, Mitume na Waumini, wanazuru kaburi la Amiril Mu’miniina Ally Bin Abi Twalib]⁽⁹⁷⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Huku ni kumkosea adabu Allaah Mola wa walimwengu wote, na kuwazulia uwongo Malaika na Mitume.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Imamu ni sawa na Mtume, amekingwa na kutenda kila aina ya dhambi na uchafu si kwa siri wala dhahiri, tangu akiwa mtoto mpaka kufa kwake, si kwa makusudi wala kukosea, kwa sababu wao Maimamu ni walinzi wa sheria na wasimamizi wake, hali yao katika hilo ni sawa Mitume]⁽⁹⁸⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Hakuna yeyote aliyekingwa na kutenda dhambi isipokuwa Mitume na Manabii peke yao, ama kulindwa kwa sheria ya Uislamu kutoingiliwa na upotoshaji au kubadilisha, jambo hili ametawalia mwenyewe Allaah Ta’alaa. Allaah anasema:

﴿إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا الذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُ لَحَافِظُونَ﴾

“Haika sisi ndio tulioteremsha Qur’an hii, na hakika sisi ndio ambao tutailinda”⁽⁹⁹⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Malaika wameumbwa ili kuwatumikia Ahlul Bayt]⁽¹⁰⁰⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Malaika wameumbwa ili kumuabudu Allaah na kumtii, na kutekeleza amri zake juu yao. Allaah anasema:

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا قُوا أَنْفُسَكُمْ وَأَهْلِيكُمْ نَارًا وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ عَلَيْهَا مَلَائِكَةٌ غِلَاظٌ شِدَادٌ لَا يَعْصُونَ اللَّهَ

مَا أَمَرَهُمْ وَيَفْعَلُونَ مَا يُؤْمَرُونَ﴾

“Enyi mlio amini, jilindeni nafsi zenu na Ahli zenu na moto ambao kuni zake ni watu na mawe. Wanausimamia (moto huo) Malaika wakali, wenye nguvu, hawamuasi Allaah kwa anayo waamrisha, na wanatenda wanayo amrishwa”⁽¹⁰¹⁾.

⁹⁷- Kitabu: [Al Furuu’ minal Kaafi] cha Al Kuleyn (Jz. 4, Uk. 580).

⁹⁸- Kitabu: [‘Aqaaidu al Imaamiyyah] cha sheikh wao Ibrahim Az Zinjaani (Jz. 3, Uk. 179).

⁹⁹- Surat Al-Hijr/9.

¹⁰⁰- Kitabu: Biharu al-Anwaar] cha Al Majlis (Jz. 26, Uk. 335).

¹⁰¹- Surat At Tahriim/6.

10- KUWAKUFURISHA MASWAHABA WOTE ISIPOKUWA WATATU TU

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Maswahaba wote waliritadi (kuucha uislamu) akiwemo Abubakar, Omar, Othman, Khalid Ibnul Walid, Mu'awiya Bin Abi Sufyan na Mughira Ibn Shu'bah, ila watu watatu]⁽¹⁰²⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Vipi lipatikane hilo na hali ya kuwa Allaah Ta'alaa anasema:

﴿لَقَدْ رَضِيَ اللَّهُ عَنِ الْمُؤْمِنِينَ إِذْ يُبَايِعُونَكَ تَحْتَ الشَّجَرَةِ فَعَلِمَ مَا فِي قُلُوبِهِمْ فَأَنْزَلَ السَّكِينَةَ عَلَيْهِمْ وَأَثَبَهُمْ فَتْحًا قَرِيبًا﴾
“Kwa hakika Allaah amewaridhia Waumini pindi walipokupa wewe Bai'a (kiapo cha utiifu) chini ya mti, na alijua yaliyomo nyoyoni mwao. Basi akateremsha utulivu juu yao, na akawalipa kwa Ushindi wa karibu”⁽¹⁰³⁾.

Na anasema:

﴿وَالسَّابِقُونَ السَّابِقُونَ أُولَئِكَ الْمُقَدَّمُونَ وَالْأَنْصَارُ وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُمْ بِإِحْسَانٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ﴾

“Na wale waliotangulia, wa kwanza, ambao ni Muhajirina na Ansaar, na waliowafuata hao kwa wema, Allaah ameridhika nao, na wao wameridhika naye, na amewaandalia wao Bustani ipitayo mito chini yake, hali ya kudumu humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa”⁽¹⁰⁴⁾.

Na anasema Subhaanah:

﴿مُحَمَّدٌ رَسُولُ اللَّهِ وَالَّذِينَ مَعَهُ أَشِدَّاءُ عَلَى الْكُفَّارِ رُحَمَاءُ بَيْنَهُمْ تَرَاهُمْ رُكَّاسًا سُجَّدًا يَبْتَغُونَ فَضْلًا مِنَ اللَّهِ وَرِضْوَانًا سِيمَاهُمْ فِي وُجُوهِهِمْ مِنْ أَثَرِ السُّجُودِ ذَلِكَ مَثَلُهُمْ فِي التَّوْرَةِ وَمَثَلُهُمْ فِي الْإِنْجِيلِ كَرَجٍ أَخْرَجَ شَطْرَهُ فَفَارَزَهُ فَاَسْتَعْلَظَ فَاَسْتَوَى عَلَى سُقُوفِهِ يُعْجَبُ الزَّعَّاعُ لِيَغِيظَ بِهِمُ الْكُفَّارَ وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ مِنْهُمْ مَغْفِرَةً وَأَجْرًا عَظِيمًا﴾

“Muhammad ni Mtume wa Allaah, na wale walio pamoja na yeye katika dini yake, ni wakali juu ya makafiri, wanahurumiana wao kwa wao, utawaona wakirukuu na kumsujudia Allaah (katika Swala zao), wakitafuta fadhila za Allaah na radhi zake. Alama za (utiifu wao) iko wazi kwenye nyuso zao kwa athari ya kusujudu. Huu ndio wasifu wao kwenye Taurati. Na wasifu katika Injili

¹⁰²- Kitabu: [Ar Raudhwa Minal Kaafi] cha Al Kulein (Jz. 8, Uk. 245).

¹⁰³- Surat Al-Fat'h/18.

¹⁰⁴- Surat At Tauba/100.

ni kama mmea uliotoa chipukizi lake, kisha ukalitia nguvu, ukawa mnene, ukasimama sawa juu ya ubuwa wake, ukawafurahisha wakulima, ili kuwakasirisha kwa ajili yao makafiri. Allaah amewaahidi walio amini na wakatenda mema katika wao msamaha na ujira mkubwa”⁽¹⁰⁵⁾.

Kuwatukana Maswahaba-Allaah awaridhie- ni kumpinga Allaah ambaye amewasifu ndani ya Qur’an na amewatakata na hayo (wanayo wasingizia), na pia ni kumkosea adabu Mtume-Swala na Salamu zimshukie- ambaye aliwafanya wao kuwa marafiki, ndugu zake na wakwe zake.

11- CHUKI YA MASHIA DHIDI YA ABUBAKAR, OMAR NA OTHMAN رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Itikadi yetu kuhusu kujitenga: Sisi tunajitenga na masanamu manne: Abubakar, Omar, Othman na Muawiyah, na tunajitenga na wanawake wanne: Aisha, Hafsa, Hindu na Ummul Hakam, na pia tunajitenga na yeyote mwenye kuwafuata hao na kuwaunga mkono, na hao ndio viumbe wa Allaah walio na shari zaidi ardhini, na kwamba haitimii Imani ya (shia) katika kumuamini Allaah na Mtume wake isipokuwa baada ya kujitenga na maadui zao]⁽¹⁰⁶⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Hakika kuwapenda Maswahaba wote ni dini na Imani, na kuwachukia ni ukafiri, unafiki na uasi. Kwa kauli yake Mtume-Swala na Salamu zimshukie-:

«خَيْرُ النَّاسِ قَرْنِي، ثُمَّ الَّذِينَ يَلُونَهُمْ، ثُمَّ الَّذِينَ يَلُونَهُمْ»

“Watu bora ni karne yangu, kisha wanao wafuatia, kisha wanao wafuatia”⁽¹⁰⁷⁾.

Na kauli Mtume-Swala na Salamu zimshukie- alipowaambia Maswahaba:

«لَا تَسُبُّوا أَصْحَابِي، فَلَوْ أَنَّ أَحَدَكُمْ أَنْفَقَ مِثْلَ أُحُدٍ، ذَهَبًا مَا بَلَغَ مُدَّ أَحَدِهِمْ، وَلَا نَصِيفَهُ»

¹⁰⁵- Surata Al-Fat-h 29.

¹⁰⁶- Kitabu: [Haqqul Yaqiin] cha sheikh wao Al-Majlis (Uk. 519).

¹⁰⁷- Kitabu: [Bukhari] (2652), na [Muslim] (2533).

“Msiwatikane Maswahaba wangu. Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake: Lau mmoja wenu alitoa sadaka ya dhahabu mfano wa mlima Uhud, asingefikia (kwa malipo) kibaba kilichotolewa na mmoja wao (hao Maswahaba) wala nusu yake”⁽¹⁰⁸⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakika Abubakar, Omar ni makafiri, ni kafiri mwenye kuwapenda wao]⁽¹⁰⁹⁾.
- **Na wanasema:** [Abubakar na Omar wamelaaniwa, na wamekufa hali ya kuwa ni makafiri, ni wenye kumshirikisha Allaah]⁽¹¹⁰⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Abubakar na Omar-Allaah awaridhie-ndio watu bora zaidi baada ya Mitume na Manabii. Wao wamebashiriwa pepo. Ni miongoni mwa watu Wa-mwanzo Waliotangulia katika uislamu. Allaah ameridhika nao na wao wameridhika nae. Ni miongoni mwa waliochukua bai’a (kiapo cha utiifu) sehemu ya Hudaybiyah. Wamejitolea katika Uislamu mali zao na nafsi zao. Ni wakwe zake Mtume-Swala na Salamu zimshukie-. Na amekufa Mtume -Swala na Salamu zimshukie-akiwa amewaridhia. Ni watu waliozikwa pembeni mwa Mtume-Swala na Salamu zimshukie-, na ni marafiki zake huko peponi.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Mtume hakumchukua Abubakar na kujificha naye pangoni isipokuwa aliogopea asije Yeye akawajulisha makafiri mahali alipojificha]⁽¹¹¹⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Mtume -Swala na Salamu hakumchukua Abubakar -Allaah amridhie- isipokuwa kwa ajili ya kutangulia kwake katika uislamu, fadhila zake na jitihada aliyonayo katika dini. Allaah anasema:

﴿إِلَّا تَصُروُ فَقَدْ نَصَرَهُ اللَّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ الَّذِينَ كَفَرُوا ثَانِيَ اثْنَيْنِ إِذْ هُمَا فِي الْغَارِ إِذْ يَقُولُ لِصَاحِبِهِ لَا تَحْزَنْ إِنَّ اللَّهَ مَعَنَا فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَيْهِ وَأَيَّدَهُ بِجُودِهِ لَمْ تَرَوْهَا وَجَعَلَ كَلِمَةَ الَّذِينَ كَفَرُوا السُّفْلَى وَكَلِمَةُ اللَّهِ هِيَ الْعُلْيَا وَاللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ﴾

¹⁰⁸- Kitabu: [Bukhari] (36673), na [Muslim] (2541).

¹⁰⁹- Kitabu: [Bihaaru Al-anwaar] cha Al-majlis (Jz. 69, Uk. 137-138).

¹¹⁰- Kitabu: [Baswaairu Ddarajaat] cha As-swaffaar (Jz. 8, Uk. 2456).

¹¹¹- Kitabu: [Tfsiiru Al-burhan] cha Hashima Al-bahraani (Jz. 2, Uk. 127).

“Tikiwa nyinyi hamtamnusuru Mtume, basi Allaah alikwisha mnusuru walipo mtoa walio kufuru, naye ni wa pili katika wawili walipokuwa katika pango, naye akamwambia sahibu yake: Usihuzunike. Hakika Allaah yu pamoja nasi. Allaah akamteremshia utulivu wake, na akamuunga mkono kwa majeshi msiyoyaona, na akalifanya neno la walio kufuru kuwa chini, na Neno la Allaah kuwa ndilo liwe juu. Na Allaah ndiye Mwenye nguvu Mwenye hekima”⁽¹¹²⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Abubakar alikuwa anaswali nyuma ya Mtume-Swala na Salamu zimshukie- na hali ya kuwa ametundika sanamu katika shingo yake analisujudia]⁽¹¹³⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Riwaya hii waislamu wote wanajua kwamba ni uzushi wa Mashia na uwongo wao usio na mipaka, pasi na kumuogopa Allaah wala kutaraji kukutana naye siku ya hesabu. Lau tujaalie riwaya hii ni sahihi, basi itakuwa ni dosari kwa Mtume-Swala na Salamu zimshukie- kabla ya Abubakar-Allaah amridhie-, **vipi itawezekana kwa Mtume ambaye ameteuliwa na Allaah na kumridhia, ashubiane na kumfanya mkwewe mtu mwenye kuabudu masanamu?! Subhaanallaah** (kutakasika na makosa ni kwa Allaah) huu ni uzushi mkubwa.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakika Omar alikuwa na maradhi ambayo hayaponi isipokuwa kwa maji ya wanaume, na kwamba bibi yake ni binti wa zinaa]⁽¹¹⁴⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Omar-Allaah amridhie- ni miongoni mwa mabwana wa Waarabu, anatokana na kabila la Kureishi, inakutana nasaba yake na nasaba ya Mtume-Swala na Salamu zimshukie- kwa babu yake wa saba Ka’b Bin Luayyi, na yeye Omar ni katika makhalifa wema wa Mtume na mmoja katika watu kumi waliopewa bishara ya pepo, naye ndiye aliyevunja ngome ya Majusi (waabudia moto huko Peshia/Iran), na wala hakuna ajabu kwa wajukuu wao (Wairani) kutunga mfano wa riwaya hizi chafu kwa mmoja katika maswahaba wa Mtume-Swala na Salamu zimshukie-.

¹¹²- Surat At-tauba/40.

¹¹³- Kitabu: [Al-anwaaru Nnu’maaniyyah] cha Ni’matullaahi Al-jazaairiy (Jz. 1, Uk. 63). Na kitabu: [As swiraatul mustaqim] cha Zainu Ddiyn An nabaatwi (Jz. 3, Uk. 28).

¹¹⁴- Kitabu: [Al-anwaaru Nnu’maaniyyah] cha Ni’matullaahi Al-jazaairiy (Jz. 1, Uk. 53).]

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Wanaitukuza siku ya Nairuz na wanafanya sherehe siku aliyowawa Omar ibnul Khatwaab -Allaah amridhie-, na wanamuita yule aliyemuuwa Omar kwa jina la: **Baba Shujaa'i Ddiyn**, na wanahimizana kuzuru kaburi lake, kama ni malipo kutokana na kumuwa Amir Al Muuminina Omar bin Khat'wab-Allaah amridhie-] ⁽¹¹⁵⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Siku ya Nairuz ni miongoni mwa Eid (sikukuu) za kishirikina ambazo wanasherehekea Majusi (waabudia moto), ama kusherehekea kwao siku ya kuuwawa Omar ni alama juu ya kuwaunga mkono kwao Majusi, na kwanini ushangea na hilo, hali ya kuwa Yeye Omar ndiye aliye sambaratisha ufalme wa babu yao Yazdajird (mtawala wa nchi ya Iran) ambaye alikuwa ni Mmajusi Muabudia moto?
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Kusoma dua ya kuwalaani masanamu mawili ya Kikureishi (Abubakar na Omar) ni katika ibada bora za kujikurubisha kwa Allaah, na wanamuita Abubakar kuwa ni Al-jibti (sanamu), na Omar ni Twaghuti (shetani)] ⁽¹¹⁶⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Yeyote atayemtusi swahaba wa Mtume-Swala na Salamu zimshukie- hasa hasa Abubakar na Omar-Allaah awaridhie-, na kuwahusisha kwenye dua hii, pamoja na kuwaita kuwa wao ni sanamu na shetani, huyo ni mwenye kuupiga vita uislamu na waislamu, vipi kwa mtu mwenye akili, anaesoma Qur'an na hadithi sahihi kisha awatukane Makhalfu wawili hawa wema Abubakar na Omar -Allaah awaridhie-?!
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Mahdi wao wa uwongo atawarudishia uhai Abubakar na Omar (kwa kuwatoa katika makaburi yao), atawasulubu na kuwachoma moto, pia atamrudishia uhai Mama wa waumini Aisha na kumpiga viboko vya adhabu ya uzinifu] ⁽¹¹⁷⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Mahdi wa shia (Muhammad bin Hassan Al-'askari) kama vilivyoeleza vitabu vya shia, ni mtu wa kubuni wala hayupo, na kwamba mashia wametunga riwaya hizo na

¹¹⁵- Kitabu: ['Aqdu Ddurar fiy baqri batwni 'Umar] cha Yasin As-swawwaaf (Uk. 120).

¹¹⁶- Kitabu: [Ihqaqul haqqi] cha Al-mar'ashiy (Jz. 1, Uk. 337).

¹¹⁷- Kitabu: [Ar raj-a'] cha Ahmad Al-ihsa'iy (Uk. 116 na 161).

kuzitengenezea taswira ya uwongo, kwa sababu ya chuki na wivu walionao dhidi ya maswahaba na wakeze Mtume.

Lakini Mahdi wa waislamu ambaye atakuja kuijaza ardhi hii usawa na uadilifu, habari zake ni kweli na ametajwa katika hadithi zilizo sahihi.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Othman -Allaah amridhie- alikuwa mzinifu na mwenye tabia za kike (khanithi), na alikuwa mpiga madufu]⁽¹¹⁸⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Othman-Allaah amridhie- ambaye Malaika walikuwa wanamuonea haya hana sifa hizo wanazotaja mashia, bali alikuwa ni mtu mwenye kupa nyongo dunia, mtu wa ibada, na msomaji sana wa Qur'an, na yeye ni mmoja kati ya maswahaba kumi walio bashiriwa pepo, na aliwahi kuoa mabinti wawili wa Mtume-Swala na Salamu zimshukie- (Ruqayyah na Ummu Kulthum), basi linatosha hili pekee kuwa ni mtukufu na mwenye fadhila.

12- MAHDI WAO WA UWONGO NA KAULI ZAO KUHUSU KUREJEA KWAKE

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Mahdi wao wa uwongo atarudi (mwisho wa dunia) ili kulipa kisasi kwa waislamu maadui wa shia, ama mayahudi na manaswara (hao si maadui zao) atasuluhisha na kuwapa amani]⁽¹¹⁹⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Riwaya hizi zinathibitisha kwamba Mahdi wao si yule wa waislamu, ambaye Mtume -Swala na Salamu zimshukie- amemtaja, kwa sababu sifa zake ni kuwa atadhihirisha alama za uislamu na itakuwa hakuna mwenye kuabudiwa ila Allaah peke yake, (lakini Mahdi wa shia atafanya suluhu na mayahudi!).
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** Jibril, Mikaeli, Kursiy, Lauhul mahfudh, na Kalamu (yenye kuandika mambo yoye ya waja), vyote hivyo vinamnyenyekeka Mahdi wa shia, kwa sababu miongoni mwa sifa zake Yeye ni Mmwagaji damu Mwenye kutiwa]⁽¹²⁰⁾.

¹¹⁸- Kitabu: [As swiraatul mustaqiim] cha Zainu Ddiyn An-nabaatwil bayadhwi (Jz. 3, Uk. 30).

¹¹⁹- Kitabu: [Bihaaru Al-anwaar] cha Al-majlis (Jz. 52, Uk. 376).

¹²⁰- Kitabu: [‘Aqaaidul Imaamiyyah] cha Muhammad Ridhwa Mudhwaffar (Uk. 102).

- **Na sisi Ahlus Sunnah tunaamini:** Jibril, Mikaeli, Kursiy, Lauhul mahfudh, na Kalamu, vyote ni viumbe wa Allaah, vinamnyenyekea yeye Subhaanah pasi na kiumbe yoyote.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Kiwiliwili cha Mahdi wa shia ni mwili wa Ki-Israel]⁽¹²¹⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Riwaya hizi ni dalili ya kwamba itikadi hizi wamezirithji kutoka kwa Mayahudi.
- **Shia Ithnaasharia wanasema kwamba:** Mahdi wa shia ataleta atakuja kuleta mambo mapya, kitabu kipya, na hukumu mpya, hatahitajia kitu chochote isipokuwa vita, hatoikubali toba ya mtu yeyote na wala hatoogopa lawama ya mwenye kulaumu]⁽¹²²⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Mahdi wa waislamu hatobadilisha kitu chochote katika sheria ya Kiislamu na atafuata mwenendo wa babu yake Mtume-Swala na Salamu zimshukie-. Imepokewa kutoka kwa Abu Said Al-khudriy-Allaah amridhie-, kwamba Mtume-Swala na Salamu zimshukie-amesema:

«يَخْرُجُ فِي آخِرِ أُمَّتِي الْمَهْدِيُّ يَسْقِيهِ اللَّهُ الْغَيْثَ، وَتُخْرِجُ الْأَرْضُ نَبَاتَهَا، وَيُعْطِي الْمَالَ صِحَاحًا، وَتَكْثُرُ الْمَأْشِيَةُ وَتَعْظُمُ الْأُمَّةُ، يَعِيشُ سَبْعًا أَوْ ثَمَانِيًا»

“Mwishoni mwa umma wangu atakuja Mahdi, Allaah atanyesheleza juu yake mvua yenye neema, ardhi itaotesha mimea yake, atagawa mali kwa usawa bila kupunja, watakithiri wanyama hoa (wanyama wa kufugwa; ng’ombe, mbuzi n.k), umma utaneemeka kwa aina mbalimbali za neema, na ataishi kwa muda wa miaka saba au minane”⁽¹²³⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakuna kilichobaki baina yetu sisi na waarabu isipokuwa ni kumwaga damu, na akaashiria kwa mkono wake juu ya shingo yake (kuwa atawachinja)]⁽¹²⁴⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Riwaya hizi ni ushahidi wa chuki ya mashia iliyojifisha katika nafsi zao dhidi ya waarabu na waislamu kwa jumla, na kwamba kuna mikononi ya watu waliojiingiza katika uislamu wakaweka riwaya ovu na za uwongo, kwa sababu ya uhasidi.

¹²¹- Kitabu: [Al-imaamul Mahdi minal wilaada ila Ddhuhuur] Muhammad Al-qazwini (Uk. 53).

¹²²- Kitabu: [Al-ghaiba] cha Muhammad An nu'maan (Uk. 154).

¹²³- Kitabu: [Al-mustadrak] cha Imam Al-hakim (8673), na [As-sahiha] hadithi namba (711).

¹²⁴- Kitabu: [Al-ghaiba] cha Muhammad An-nu'maan.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Mahdi wao atauvunja msikiti mtakatifu wa Makka (Al-masjidul Haraam) na msikiti wa Mtume huko Madina (Al-masjidu Nnabawi), na atahukumu kwa kutumia sheria ya watu wa Daud, na atamsemesha Allaah kwa jina lake la Ki-ibrania. Ana isitoshe atawauwa watu theluthi mbili ya watu wa duniani]⁽¹²⁵⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Hakika vitendo vyote vya Mahdi wa kishia, vinajulisha kwamba huyo ni Masih Dajjal na wala yule Mahdi aliyetajwa na Mtume-Swala na Salamu zimshukie-.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakuna Jihad isipokuwa baada ya kutoka Mahdi pangoni mwake]⁽¹²⁶⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Ndio maana huwezi kupata kwa mashia athari yoyote ya kupigana Jihad na kuikomboa miji kutoka kwa makafiri, wala hapati katika historia kiongozi wa shia aliyeongoza jeshi la shia kuvamia nchi za makafiri, na kuzifanyia kazi fat-wa hizi ni kuivunja sheria ya uislamu na kuharibu msingi wake.

13- KUVUKA KWAO MIPAKA KATIKA KUABUDU MAKABURI

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakika kuzuru kaburi la Hussein bin Ally ni bora kuliko kuhiji nyumba tukufu (Makka), bali wenye kumzuru Hussein wametakasika, na watu walio simama Arafa kuna miongoni mwao watoto wa zinaa]⁽¹²⁷⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Kuhiji nyumba tukufu ya Makka ni kutekeleza nguzo ya tano ya Kiislamu, na imekuja katika hadithi:

«وَالْحَقُّ الْمَبْرُورُ لَيْسَ لَهُ جَزَاءٌ إِلَّا الْجَنَّةُ»

“Hija yenye kutakata haina malipo isipokuwa pepo”⁽¹²⁸⁾.

Ama kuzuru kaburi la Hussein au makaburi mengine ya Waislamu, na kuhusisha malipo ya kiwango fulani hiyo ni bidaa. Na watu walio simama viwanja vya Arafa inatosha kuwa ni fadhila kwao kwamba Allaah anajifakhiri nao katika siku hiyo tukufu.

¹²⁵- Kitabu: [Bihaarul anwaar] (Jz. 52, Uk. 338), [Usuulul kaafi] (Jz. 1, Uk. 397), [Al-ghaiba] (Uk. 51).

¹²⁶- Kitabu: [Wasaaailu Sshia] cha Al-hurruul ‘Aamiliy (Jz. 11, Uk. 37).

¹²⁷- Kitabu: [Bihaarul Anwaar] cha Al-majlis (Jz. 98, Uk. 85).

¹²⁸- Kitabu: [Bukhari] (1773) na [Muslim] (1349).

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Kuzuru kaburi la Hussein bin Ally ni sawa na kufanya Hija mara Milioni Mbili, na Umra Milioni Mbili, na kupigana Jihadi mara Milioni Mbili, na malipo ya kila Hija moja, Umra, na Jihadi moja, ni sawa na malipo ya mtu aliyefanya Hija, Umra, na kupigana Jihadi pamoja na Mtume-Swala na Salamu zimshukie- na Maimamu wema (wa shia)]⁽¹²⁹⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Malengo ya Shia Raafidhwa kutunga riwaya hizi ni kujaribu kuwazuia waislamu wasiende kuhiji msikiti mtakatifu wa Makka, na kutaka kuigeuza Hija na Umra kwa kuwaelekeza watu kwenda kwenye makaburi yanayo abudiwa kinyume na Allaah Ta'alaa, Allaah atukinge.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** Karbala ndio ardhi iliyotakasika zaidi katika uislamu, na mahali patukufu kuliko Makka, Madina na Baytul Maqdis (Palestina)]⁽¹³⁰⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Hakika misikiti mitatu: msikiti wa Makka, Madina, na Baytul Maqdis, zimekuja hadithi kutoka kwa Mtume-Swala na Salamu zms hukie- kuelezea fadhila zake na ubora wa kuswali ndani yake, ama Karbala hakuna yeyote katika waislamu aliyetaja fadhila zake, na huwezi kupata jambo hili isipokuwa katika dini ya shia, ambao wanapingana na itikadi za waislamu katika misingi ya dini na matawi yake.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Kula udongo wa kaburi la Hussein ni ponyo la kila maradhi]⁽¹³¹⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Hii ni alama ya kuvuka mipaka kuhusu Hussein -Allaah amridhie-, mpaka wamempa daraja la kuabudiwa, na wakaegemeza ponyo katika udongo wa kaburi lake.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Wakimzulia Abu Abdillahi (Ja'far Swaadiq) kwamba amesema: "Wallaahi, lau ningewasimulia fadhila za kumzuru Hussein na utukufu wa kaburi lake, mngeacha kwenda kuhiji (Makka), na asingehiji mtu yeyote miongoni mwenu, kuangamia ni kwako, hivi hujui kwamba Allaah ameufanya mji wa Karbala kuwa Mtakatifu, Umebarikiwa, na Wenye amani, kabla ya Makka?!]⁽¹³²⁾.

¹²⁹- Kitabu: [Nuurul 'ain fiy ziyaarat qabrul Hussein] cha Muhammad Istwahbaanaty (Uk. 265).

¹³⁰- Kitabu: [Maswaabihul jinaan] cha sheikh wao Abbas Al-kaashani (Uk. 360).

¹³¹- Kitabu: [Al-mazaar] cha Al-mufid (Uk. 125).

¹³²- Kitabu: [Kaamilu Zziyaraat] cha sheikh wao Ibn Quulawaihi al-qummi (Uk. 449).

- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Inatosha kujibu Shubha hizi kwa aya:

﴿وَلِلّٰهِ عَلَى النَّاسِ حُجُّ الْبَيْتِ مَنِ اسْتَطَاعَ اِلَيْهِ سَبِيْلًا﴾

“Na kuna haki aliyowajibisha Allaah juu ya watu kuhiji Nyumba hiyo, kwa yule awezaye njia ya kwendea”⁽¹³³⁾.

Vipi tuache kutekeleza nguzo ya tano ya uislamu kwa Kwenda kuzuru kaburi la Hussein-Allaah amridhie-?! Je, huku si kuvunja msingi wa dini ya uislamu?!

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Kuswali kwenye makaburi ya viongozi wao, ni bora kuliko kuswali katika misikiti, bali wanasema: Malipo ya swala moja katika Masjid Ally bin Abi Twalib ni sawa na swala mbili katika Masjid al-Haraam (Makka)]⁽¹³⁴⁾.

- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Allaah Ta’alaa anasema:

﴿وَأَنَّ الْمَسَاجِدَ لِلّٰهِ فَلَا تَدْعُوا مَعَ اللّٰهِ أَحَدًا﴾

“Hakika misikiti ni ya kuabudiwa Allaah, basi msiabudu humo asiyekuwa Allaah”⁽¹³⁵⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Eid (sikukuu) kubwa katika uislamu si Eid al-Fitr na Eid al-Adh’ha, bali ni Eid ya Ghadir]⁽¹³⁶⁾.

- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Allaah amewachagulia waislamu Eid (sikukuu) mbili: Eid al-Fitr na Eid al-Adh’ha, ama Eid ya Ghadir si katika Eid (sikukuu) za waislamu.

¹³³- Surat Aali Imraan/97.

¹³⁴- Kitabu: [Manhaju Sswaalihin] cha sheikh wao Ally Sistani (Jz. 1, Uk. 187).

¹³⁵- Surat Al-jinni/18.

¹³⁶- Kitabu: [Eid al-Ghadir] cha sheikh wao Muhammad Shiraz (Uk. 11).

14- KUWAPENDA KWAO MAKAFIRI NA KHIYANA YAO DHIDI YA AHLUL BAYT

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Miongoni mwa mambo waliyo laumiwa watu wa mji wa Kufa, ni kwamba wao wamemchoma mkuki Hassan bin Ally na wamemuuwa Hussein baada ya kuwa wamemuita]⁽¹³⁷⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Allaah Ta'alaa anasema:

﴿وَشَهِدَ شَاهِدٌ مِّنْ أَهْلِهَا﴾

“Na akatoa Ushahidi miongoni mwa jamaa zake”⁽¹³⁸⁾.

Huku ni kukiri kwa wazi kabisa kwamba wao ndio walioacha kuwanusuru watukufu hawa wa Ahlul bayt Hassan na Hussein-Allah awaridhie-.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakika Hussein aliomba dua akasema: “Ewe Allaah, tuhukumu baina yetu sisi na baina ya watu ambao wametuita ili watupe nusra, kisha wametuuwa”]⁽¹³⁹⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Huu ni uthibitisho wa wazi kwamba shia wa Kufa ndio waliomuita Hussein, kisha wakamsaliti na wakamuuwa.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** Hussein amesema: “Hakika watu hawa (wa mji wa Kufa) wameni ogopesha, hizi ni barua za watu wa Kufa (wameniita), kisha wao wametaka kuniuwa”⁽¹⁴⁰⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Huu ni ushahidi mwingine, kwamba mashia wa mji wa Kufa walimpa bai'a (kiapo cha utiifu) Hussein, kisha wakamgeuka na kumuuwa.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** Ally bin Hussein -Allaah amrehemu- aliwaona watu wa Kufa wanalia kwa uchungu, akawaambia: **Hivi mnalia kwa ajili yetu! Kwani ni nani alituuwa?**⁽¹⁴¹⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Hii ni tuhuma ya wazi kwa Zainul 'Aabidiin Ally bin Hussein dhidi ya watu wa mji wa Kufa, kwamba wao ndio waliompa baia baba yake Hussein bin Ally -Allaah amridhie-, kisha wakamuuwa na wakaanza kumlilia.

¹³⁷- Kitabu: [Tareikh al-Kufa] (Uk. 113).

¹³⁸- Surat Yusuf/26.

¹³⁹- Kitabu: [Muntahaa al-Aamal] (Jz. 1, Uk. 535).

¹⁴⁰- Kitabu: [Maqtalul Hussein] cha

¹⁴¹- Kitabu: [Nafsul mahmum] cha Abbas al-qummi (Uk. 357).

- **Na miongoni mwa kauli za masheikh wa Shia Ithnaasharia:** [Ni wajibu kusaidia majeshi ya maadui waliovamia Nchi za Kiislamu, ili wapate ushindi dhidi ya waislamu]⁽¹⁴²⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Hakika uvamizi uliofanywa na maadui katika nchi ya Iraq, umetubainishia kwamba mashia kawaida yao ni kumsaidia kila mwenye kushambulia miji ya waislamu (masunni), wala hawabebi silaha kuwanusuru waislamu hapana. Ndio maana aliyewahi kuwa Naibu Rais wa Iran Muhammad Ally Abtwahiy aliwahi kusema: **“Lau si Iran kuisaidia nchi ya Marekani usingeanguka mji wa Kabul wala Baghdad”**⁽¹⁴³⁾.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Waislamu wanaopigana na kulinda mipaka hao ni wauaji wa duniani na akhera, na mashahidi wa kweli ni Shia Imaamiyyah hata kama watakufa katika vitanda vyao]⁽¹⁴⁴⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Kauli hii ni ushahidi wa wazi juu ya kwamba mashia wanawakufurisha waislamu, hata watu wanaopigana Jihad ili neno la Allaah (Laa ilaaha illa Lahu) liwe juu hao ni wauaji wa duniani na akhera, kwa mtazamo wa shia.

15- CHUKI YAO DHIDI YA MAKKA NA MADINA

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakika watu wa Makka wanamkufuru Allaah waziwazi, na watu wa Madina ni waovu zaidi kuliko watu wa Makka kwa mara sabini]⁽¹⁴⁵⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Hakika Makka imeombewa dua na Nabii Ibrahim-alaihis salaam- akasema:

﴿وَإِذْ قَالَ إِبْرَاهِيمُ رَبِّ اجْعَلْ هَذَا بَلَدًا آمِنًا وَارْزُقْ أَهْلَهُ مِنَ الثَّمَرَاتِ مَنْ آمَنَ مِنْهُمْ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ قَالَ وَمَنْ كَفَرَ فَأُمَتِّعُهُ قَلِيلًا ثُمَّ أَضْطَرُّهُ إِلَىٰ عَذَابِ النَّارِ وَبِئْسَ الْمَصِيرُ﴾

¹⁴²- Fatwa ya sheikh wao mkubwa Sistaan [4/3/2003] na akatia nguvu kauli hiyo sheikh wao Muhammad Al-mahriy kwa kusema: “Fatwa zinazotoka kwa masheikh wa kutegemewa katika huko Iraq, zinazohimiza wajibu wa kupigana Jihad dhidi ya majeshi ya kigeni ambayo yanakusudia kuipiga nchi ya Iraq hazina hoja yoyote, hiyo ni Taqiyya na hofu ya kuogopea uhai...”. (Ijumaa ya 27/9/2002m).

¹⁴³- Tazama kitabu: [Maadha ta’rifu ‘an Hizbillaah] cha Ally Swadiq (Uk. 208).

¹⁴⁴- Kitabu: [Tahdhiibul ahkaam] cha At-tuusi (Jz. 6, Uk. 98).

¹⁴⁵- Kitabu: [Usuulu al-kaafi] cha Al-kulein (Jz. 2, Uk. 410).

“Na kumbuka wakati aliposema Ibrahim: Ewe Mola wangu Mlezi! Ufanye mji huu wa Makka uwe wenye amani, na uwaruzuku watu wake matunda, wale wanao muamini Allaah na siku ya Mwisho. Akasema: Na mwenye kukufuru pia nitamstarehesha kidogo, kisha nitamsukumiza kwenye adhabu ya Moto. Na ubaya wa marejeo na makazi ni huo Moto”⁽¹⁴⁶⁾.

Ama watu wa Madina, Allaah amewatakaswa kwa kauli yake:

﴿وَالسَّابِقُونَ السَّابِقُونَ أُولَئِكَ الْمُقَدَّمُونَ وَالْأَنْصَارُ وَالَّذِينَ اتَّبَعُوهُمْ بِإِحْسَانٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ وَأَعَدَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ﴾

“Na wale walio tangulia, wa mwanzo, katika Muhajirina na Answari, na waliowafuata kwa wema, Allaah ameridhika nao, na wao wameridhika naye, na amewaandalia Bustani ambazo inapita chini yake mito, hali ya kudumu humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa”⁽¹⁴⁷⁾.

Na Mtume-Swala na Salamu zimshukie- amesema:

«إِنَّ الْإِيمَانَ لِيَأْرُزُ إِلَى الْمَدِينَةِ كَمَا تَأْرُزُ الْحَيَّةُ إِلَى جُحْرِهَا»

“Hakika Imani itajikusanya katika mji wa Madina kama nyoka anavyo jikusanya katika shimo lake”⁽¹⁴⁸⁾.

Pia amesema:

«لَا يَكِيدُ أَهْلَ الْمَدِينَةِ أَحَدٌ، إِلَّا انْمَاعَ كَمَا يَنْمَاعُ الْمَلْحُ فِي الْمَاءِ»

“Hatopanga njama mbaya mtu yeyote dhidi ya watu wa Madina, isipokuwa atayeyuka kama inavyoyeyuka chumvi katika maji”⁽¹⁴⁹⁾.

Allaah atamuadhibu kwa haraka bila kumchelewesha.

¹⁴⁶- Surat Al-Baqara/126

¹⁴⁷- Surat At-Tauba/100.

¹⁴⁸- Kitabu: [Bukhari] (1876) na [Muslim] (147).

¹⁴⁹- Kitabu: [Bukhari] (1877).

16- CHUKI YAO DHIDI YA MISRI NA SHAM

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakika watu wa Misri wamelaaniwa kupitia ulimi wa Nabii Daud, wakafanywa miongoni mwao kuwa Nyani na Nguruwe].
- **Na wanasema:** [Allaah hakuwakasirikia Wana wa Israel isipokuwa aliwaingiza Misri, na wala hawakuwaridhia isipokuwa aliwatoa humo].
- **Na wanasema:** [Amesema Abu Ja'far (imamu wao): Hakika mimi nachukia kula chakula chochote kilichopikwa na vyombo vya Misri, na wala sipendi kupaka kichwa changu na udongo wake, nachelea utaniambukiza udhalili, na kuniondoshea wivu. Piteni Misri na wala msifanye ukazi (msiishi humo). Nadhania pia alisema: Kuisi katika nchi hiyo kunamuondolea mtu wivu]⁽¹⁵⁰⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Sababu ya Mashia kuichukia nchi ya Misri na kuwachukia watu wake, ni kwamba nchi hiyo tangu zama za swahaba 'Amru Ibnul 'Aasw-Allaah amridhie- imekuwa ni ngome ya Ahlus Sunnah, na itaendelea hivyo kwa idhini ya Allaah.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Sham ni nchi nzuri lakini watu wake ni waovu, na watu wa Roma (Italy) ni makafiri lakini hawakutupiga vita, na watu wa Sham wamekufuru na wametupiga vita. Na wala msiwaite watu wa Sham, lakini waiteni watu wa Shu'mu (wenye nuksi/nuhusi)]⁽¹⁵¹⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Kuna hadithi nyingi zimekuja kuelezea fadhila za watu wa Sham, miongoni mwa hizo ni: **"Wakifisidika watu wa Sham basi hakuna kheri kwenu"**⁽¹⁵²⁾.

17- KULA WATU WA VILEMBA MALI YA KHUMUS (SEHEMU MOJA KATIKA TANO)

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Mali ya Khumus iliyo husishwa kupewa Ahlul bayt (Jamaa wa nyumba ya Mtume), wanastahiki kupewa masheikh (wa shia) wenye vilemba vikubwa, wakidai kwamba wanachukua kwa niaba ya Imamu wao (Mahdi) aliyejificha pangoni]⁽¹⁵³⁾.

¹⁵⁰- Kitabu: [Tafsirul Qummi] cha Ally Al-Qummi (Jz. 2, Uk. 241), [Tafsiru al-Burhan] cha Hashim al-Bahraani (Jz. 1, Uk. 456), [Furuul-Kaafi] cha Al-Kuleini (Jz. 6, Uk. 501) na kitabu: [Bihaarul-Anwaar] (Jz. 60, Uk. 211).

¹⁵¹- Kitabu: [Tafsiru al-Burhan] cha Hashim al-Bahraani (Jz. 1, Uk. 456), [Usuul al-Kaafi] cha Al-Kulein (Jz. 2, Uk. 410), na [Tafsirul Qummi] cha Ally Al-Qummi (Jz. 2, Uk. 241),

¹⁵²- Kitabu: [Musnad Ahmad] (15596).

¹⁵³- Kitabu: [Wasaaailu Sshia] (Jz. 6, Uk. 383).

- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Hakika mali ya Khumus haipatikani isipokuwa katika vita, na si kama wanavyofanya Mashia hivi leo.
Allaah Ta'alaa anasema:

﴿وَأَعْلَمُوا أَنَّمَا غَنِمْتُمْ مِنْ شَيْءٍ فَإِنَّ لِلَّهِ خُمُسَهُ وَلِلرَّسُولِ وَلِذِي الْقُرْبَىٰ﴾

“Na Jueni kwamba ngawira yoyote mnayoipata (kutoka kwa maadui zenu), basi Khumus⁽¹⁵⁴⁾ ni kwa ajili ya Allaah na Mtume wake, na Jamaa wa karibu (wa Mtume)”. [Surat Al-Anfaal/41].

Wala hakuna dalili yoyote si kwenye Qur'an wala katika Sunnah, imeruhusu kupewa mali ya Khumus watu wa kawaida.

18- MADAI YAO KWAMBA KUJIPIGA MAKOFI USONI NA KUJIKATA KWA VISU NA MAPANGA MWILINI NI MIONGONI MWA IBADA KUBWA

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakika kujipiga makofi, kujichoma kwa visu na mapanga, kuvaa nguo nyeusi, na kunyanyua sauti za kuomboleza katika siku ya 'Ashuraa (tarehe 10 Muharram), ni miongoni mwa ibada kubwa ya kujikurubisha kwa Hussein, bali ni katika mambo yanayosifiwa]⁽¹⁵⁵⁾.

- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Imekuja katika hadithi:

«لَيْسَ مِنَّا مَنْ لَطَمَ الْخُدُودَ، وَشَقَّ الْجُيُوبَ، وَدَعَا بِدَعْوَى الْجَاهِلِيَّةِ»

“Si katika sisi mwenye kujipiga makofi usoni, kuchana nguo, na akaomba kwa maombi Jaahiliyyah ((maneno wakiyo yasema washirikina kabla ya Uislamu)”. [Bukhari] (1294).

Na kauli yake Mtume-Swala na Salamu zimshukie:-

«أَنَا بَرِيءٌ مِنَ الصَّالِقَةِ، وَالْحَالِقَةِ، وَالشَّاقَةِ»

“Mimi najiweka mbali na mwanamke Mwenye kunyanyua sauti kwa kuomboleza wakati wa msiba, Mwenye kunyoa nywele zake, na Mwenye kuchana nguo zake”. [Muslim] (104).

¹⁵⁴- Mali inayopatikana kutoka kwa maadui (Ngawira) inagawanywa mafungu matano, mafungu manne kwa ajili ya askari, na fungu moja lililosalia litagawanywa sehemu tano:

- **Ya kwanza:** Allaah na Mtume wake, (itawekwa kwenye manufaa ya Waislamu wote).

- **Ya pili:** Jamaa wa karibu wa Mtume -Swala na Salamu zimshukie-.

- **Ya tatu:** Ni ya Mayatima.

- **Ya nne:** Ni ya Masikini.

- **Ya tano:** Ni ya msafiri aliyemalizikiwa na matumizi ⁴¹

¹⁵⁵- Tazama: [Fat-wa ya Muhammad Kaashiful Ghitwaa, Ar Ruuhani, Tibrizi na masheikh wengine].

19- KUHIMIZA KWAO MASHIA JUU YA NDOA YA MUTAA' PAMOJA NA KUFAA KUSTAREHE NA WANAWAKE MAKAHABA

➤ **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Inawezekana kwa mtu kuoa ndoa ya Mut'aa mpaka (wanawake) Elfu Moja, kwa sababu mwanamke wa Mut'aa hapewi talaka wala harithiwi, bali ni mwanamke wa kukodisha tu]⁽¹⁵⁶⁾.

▪ **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Allaah Ta'alaa amesema:

﴿وَالَّذِينَ هُمْ لِأُزُوجِهِمْ حَافِظُونَ ** إِلَّا عَلَى أَزْوَاجِهِمْ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ فَإِنَّهُمْ غَيْرُ مَلُومِينَ ** فَمَنْ أَبْتَغَى وَرَاءَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الْعَادُونَ﴾

“Na ambao wanazilinda tupu zao * Isipokuwa kwa wake zao na wajakazi waliomilikiwa na mikono yao ya kulia. Hao Waumini hawana lawama wala makosa kuwaingilia na kujistarehesha nao * Lakini mwenye kutaka kujistarehesha kinyume ya haya, hao ni wenye kuruka mipaka”⁽¹⁵⁷⁾.

Hapa amevuliwa mke wa kudumu na mjakazi tu, ndio umeruhusiwa kustarehe nao. Ama ndoa ya mutaa' Mtume -Swala na Salamu zimshukie- ameharamisha, imekuja hadithi katika sahihi Muslim (1406): Kutoka kwa Rabii Bin Sabura Al-Juhaniy, kwamba baba yake alimsimulia: Yeye alikuwa pamoja na Mtume -Swala na Salamu zimshukie- akasema:

«يَا أَيُّهَا النَّاسُ، إِنِّي قَدْ كُنْتُ أَذْنْتُ لَكُمْ فِي الْإِسْتِمْتَاعِ مِنَ النِّسَاءِ، وَإِنَّ اللَّهَ قَدْ حَرَّمَ ذَلِكَ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ، فَمَنْ كَانَ عِنْدَهُ مِنْهُنَّ شَيْءٌ فَلْيُخْلِ سَبِيلَهُ، وَلَا تَأْخُذُوا مِمَّا آتَيْنَاهُمْ شَيْئًا»

“Enyi watu, hakika nilikuwa nimewaruhusu kustarehe na wanawake (mutaa'), na (hivi sasa) Allaah ameharamisha (jambo hilo) mpaka siku ya kiama, yule ambaye ana mwanamke miongoni mwa hao amwache, wala msichukue chochote katika vile mlivyowapa (katika mahari)”⁽¹⁵⁸⁾.

➤ **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakika mtoto wa mutaa' ni bora zaidi kuliko mtoto wa mke wa (ndoa ya) kudumu]⁽¹⁵⁹⁾.

▪ **Na sisi Ahlus Sunnah wanasema:** Maneno haya ni alama ya kuhimiza kwao mutaa' na pamoja na Uislamu kuharamisha jambo hilo.

¹⁵⁶- Kitabu: [Al-istibswaar] cha Abu Ja'far At Tuusi (Jz 3, Uk. 155).

¹⁵⁷- Surat Al-Mu'minun/5-7.

¹⁵⁸- Kitabu: [Muslim] (1406).

¹⁵⁹- Kitabu: [Manhaju Sswadiqiin] cha sheikh wao Mulla-Fat-hullaah Al-Kaashani (Uk. 356).

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Inafaa kufanya mutaa' na wanawake makahaba, na wanawake walio mashuhuri kwa uasherati...] ⁽¹⁶⁰⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Allaah Ta'alaa amesema:

﴿الزَّانِي لَا يَنْكِحُ إِلَّا زَانِيَةً أَوْ مُشْرِكَةً وَالزَّانِيَةُ لَا يَنْكِحُهَا إِلَّا زَانٍ أَوْ مُشْرِكٌ وَحُرِّمَ ذَلِكَ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ﴾

“Mwanamume mzinifu hamwoi ila mwanamke mzinifu au mwanamke mshirikina. Na mwanamke mzinifu haolewi ila na mwanamume mzinifu au mshirikina. Na hayo yameharamishwa kwa Waumini” ⁽¹⁶¹⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Mke wa ndoa ya mutaa' haingii katika hesabu ya wake wanne, kwa sababu yeye hhapewi talaka, wala harithiwi, bali huyo ni mwanamke wa kukodisha] ⁽¹⁶²⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Huu ni ushahidi kwamba ndoa ya mutaa' si ndoa ya kisheria, lau ingelikuwa ni ndoa ya kisheria kungepatikana ndani yake kurithi, talaka, na haki nyingine anazostahiki mwanamke kuzipata.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Inajuzu kufanya mutaa' na mwanamke mrembo, hata kama ameolewa (mke wa mtu) au ni kahaba] ⁽¹⁶³⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Riwaya hizi zote zinahamasisha uzinifu, na matendo ya haramu. Tunamuomba Allaah atupe afya na atusalimishe.
Na kama si kuhamasisha uzinifu vipi iwe inafaa kufanya mutaa' na mwanamke aliye ndani ya ndoa?!
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Kiwango cha chini cha kufanya mutaa' ni mtu kufanya mutaa' angalau mara moja (katika maisha yake)] ⁽¹⁶⁴⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Inatosha kwa riwaya hizi kuwa ni Ushahidi wa kwamba mwanamke hana thamani yoyote katika dini ya shia.

¹⁶⁰- Kitabu: [Bihaa al-Anwaar] cha Al-Majlis (Jz. 100, Uk. 319-320).

¹⁶¹- Surat An Nuur/3.

¹⁶²- Kitabu: [Al-Furru' minal Kaafi] cha Al-Kuleini (Jz. 5, Uk. 415).

¹⁶³- Kitabu: [Al-Furru' minal Kaafi] cha Al-Kuleini (Jz. 5, Uk. 462).

¹⁶⁴- Kitabu: [Al-Furru' minal Kaafi] cha Al-Kuleini (Jz. 5, Uk. 460).

20- TAQIYYA NA UWONGO NDIO MSINGI WA DINI YAO

- **Shia Ithnaasharia wanaamini kwamba:** [Ni lazima shia kutumia Taqiyya; na maana ya Taqiyya ni: kudhihirisha tafauti na Imani yako, au kama alivyoelezea mmoja wa maulamaa wao: Maana ya Taqiyya ni: Kusema au kufanya kinyume na itikadi yako, ili kuilinda nafsi yako na madhara au kuhifadhi heshima yako]⁽¹⁶⁵⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Taqiyya ya Shia Imaamiyyah ni uwongo usio na shaka, imekuja hadithi kutoka kwa Mtume-Swala na Salamu zimshukie- inayokataza kusema uwongo:

«وَمَا يَزَالُ الرَّجُلُ يَكْذِبُ وَيَتَحَرَّى الْكَذِبَ حَتَّى يُكْتَبَ عِنْدَ اللَّهِ كَذَّابًا»

“Ataendelea mtu kusema uwongo na kudumu kati uwongo, mpaka atahukumiwa mbele ya Allaah kuwa Muwongo”⁽¹⁶⁶⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Asilimia tisa ya kumi ya dini ya Shia ipo katika Taqiyya, hana dini yule asiye na Taqiyya]⁽¹⁶⁷⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Mtume-Swala na Salamu zimshukie- amesema: **“Hakika ukweli unaongoza kwenye wema, na wema unaongoza kwenye pepo, ataendelea mtu kuwa mkweli, na kusifika na tabia ya ukweli mpaka atahukumiwa mbele ya Allaah kuwa ni Mkweli”⁽¹⁶⁸⁾.**
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakika nyinyi mashia mpo katika dini ambayo yule mwenye kuficha (itikadi) yake, Allaah atampa ushindi, na yule mwenye kudhihirisha (itikadi) yake, Allaah atamdhalilisha]⁽¹⁶⁹⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Maneno haya ni ushahidi kwamba kuenea kwa dini ya shia ni lazima kuficha itikadi zake, kwa sababu lau watabainisha kwa watu ukweli wa dini yao, hakuna muislamu atayekubali.

¹⁶⁵- Kitabu: [Bukhari] (6094) na [Muslim] (2607).

¹⁶⁶- Kitabu: [As Shiia' fil Miizaan] (Uk. 48).

¹⁶⁷- Kitabu: [Usuul al-Kaafi] (Jz. 2, Uk. 217).

¹⁶⁸- Kitabu: [Bukhari] (6094) na [Muslim] (2607).

¹⁶⁹- Kitabu: [Usuul al-Kaafi] cha Al-Kulein (Jz. 2, Uk. 222).

21- KUWAKUFURISHA KWAO WAISLAMU WOTE NA KUWACHUKIA

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakuna katika dini ya uislamu isipokuwa sisi na wao, (Maimamu wa shia na wafuasi wao tu)]⁽¹⁷⁰⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Kila mwenye kusema: (Laa Ilaaha illa Llaahu, Muhammad rasuulu Llaahi), mwenye kutamka kwa ulimi wake na kukiri kwa moyo wake kwamba: Hapana mwenye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah na Muhammad-Swala na Salamu zimshukie- ni Mtume wake, na akatekeleza masharti ya shahada mbili hizo, huyo ni muislamu, ambaye imekingwa damu yake, mali na heshima yake.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakika kila ambaye si Shia Ithnaasharia, au hakuamini Maimamu kumi na mbili wa kishia, au akampinga mmoja kati yao, huyo ni kafiri, na huko akhera makazi yake ni motoni]⁽¹⁷¹⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Lau ingelikuwa kuamini Maimamu kumi na mbili ni sababu ya kuingia peponi, na kuacha kuwaamini wao ni sababu ya kuingia motoni, basi Allaah angeli bainisha hilo katika Qur'an, na angelitaja hilo Mtume wake-Swala na Salamu zimshukie- katika hadithi.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakika miongoni mwa yenye kupatiwa faida katika hadithi mbalimbali zilizokuja kuelezea hukumu ya ukafiri na ushirkina huko akhera: hukumu hiyo itampata yule asiyekuwa shia Ithnaasharia]⁽¹⁷²⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Atayetamka kwa ulimi wake na kukiri kwa moyo wake: Laa ilaaha illa Llaahu, Muhammad Rasuulu Llaahi, (**hakuna mwenye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allaah, na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah**), na akafa juu ya Imani hiyo, basi hukumu yake ipo kwa Allaah; akitaka atamuadhibu, na atamsamehe, sisi hatushuhudii kwa muislamu yeyote kuwa wa peponi au motoni, isipokuwa yule aliyetajwa na Allaah au Mtume wake-Swala na Salamu zimshukie-.

¹⁷⁰- Kitabu: [Usuul al-Kaafi] (Jz. 1, Uk. 223-224).

¹⁷¹- Kitabu: [Jaami'u ahaadithi Sshii'a] cha Sheikh wao BaruuJurdi (Jz. 1, Uk. 429).

¹⁷²- Tanqiihu al-Maqaal] cha Abdullaahi Al-Maamaqani (Jz. 1, Uk. 208).

22- CHUKI YAO DHIDI YA AHLUS SUNNAH NI ZAIDI YA WASIFU

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakika watu wote ni watoto wa zinaa isipokuwa mashia]⁽¹⁷³⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Huku ni kuwatuhumu waislamu wote dhambi ya uzinifu, na kwamba wao ni watoto wa zinaa kwa sababu wao si mashia. Itikadi hii inafanana na itikadi ya mayahudi, ambao wamesema:

﴿نَحْنُ أَبْنَاءُ اللَّهِ وَأَحِبُّهُ﴾

“Sisi bi wan awa Allaah na vipenzi vyake”⁽¹⁷⁴⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakuna mtoto yeyote anayezaliwa isipokuwa anahudhuria mmoja miongoni mwa wafuasi wa Iblis, akijua kwamba mtoto huyo ni miongoni mwa shia (wafuasi) wetu, anamkinga na shetani. Lakini akijua kwamba mtoto huyo si katika shia (wafuasi) wetu, shetani anaweka kidole chake katika duburi yake (tundu ya nyuma), na anakuwa Khanithi (mwenye vitendo vya kike), na kama akiweka katika tupu ya mtoto wa kike anakuwa ni malaya]⁽¹⁷⁵⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Riwaya hizi zinabainisha chuki yao iliyojificha dhidi ya waislamu wasiokuwa mashia, kwa kuwatuhumu wanaume wote masuni kwamba wanafanya vitendo vya liwati (kuendana kinyume ya maumbile), na wanawake wao ni Malaya. Allaah atukinge.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Naaswib (sunni) ni halali kumwaga damu yake, na wanaitaja riwaya za uwongo kutoka kwa Jafar Swadiq amesema: (Ukiweza kumuangushia ukuta au kumzamisha kwenye maji bila kukuona mtu yeyote fanya hivyo), akauliza: vipi kuhusu mali yake? Akasema: (langamize kiasi unachoweza)]⁽¹⁷⁶⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Naaswib ni adui wa Ahlul Bayt, lakini shia Imaamiyyah wanawaita Ahlus Sunnah kwa jina hilo, kwa sababu wao wanamtanguliza Abubakar, Omar na Uthman katika Ukhalifa juu ya Ally-

¹⁷³- Kitabu: [Ar raudhwa minal Kaafi] cha Al Kulein (Jz. 8, Uk. 285).

¹⁷⁴- Surat Al-Maida/18.

¹⁷⁵- Kitabu: [Tafsiir al-'Ayyaash] cha Muhammad al-'Ayyaash (Jz. 2, Uk. 218).

¹⁷⁶- Kitabu: [Wasaailus Shiaa'] cha Al-Hurru'l 'Aamiliy (Jz. 18, Uk. 463).

Allaah awaridhie wote-, kwa sababu hii wanahalalisha kumwaga damu yao na kupora mali yao.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Chukua mali ya Naaswib (muislamu asiyekuwa shia) popote utakapo ikuta, na tupatie sisi Khumus (fungu moja ya tano)]⁽¹⁷⁷⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Hii ni riwaya nyingine inahalalisha kuchukua mali ya Ahlus Sunnah na kumwaga damu yao, pamoja dini ya kiislamu imekuja kuhifadhi haki tano za muislamu (nafsi, dini, heshima, mali na akili).
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Matendo mema ya Ahlus Sunnah (sunni) siku ya kيامa watapewa mashia, matendo maovu ya mashia siku ya kيامa watapewa sunni, kisha watatupwa katika moto]⁽¹⁷⁸⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Kwanini iwe hivyo, na Allaah anasema:

﴿كُلُّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ رَهِينَةٌ﴾

“Kila nafsi imefungwa na kuwekwa rehani kwa ilichokitenda”⁽¹⁷⁹⁾.

Na anasema Subhaanah:

﴿وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ﴾

“Wala haitabeba nafsi yenye dhambi, dhambi za nafsi nyingine”⁽¹⁸⁰⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Ahlus Sunnah ni najisi na ni halali kumwaga damu yao na kupora mali yao, na wao watakaa motoni milele bila kutoka]⁽¹⁸¹⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Mtume-Swala na Salamu zimshukie-anasema:

«إِنَّ الْمُؤْمِنَ لَا يَنْجُسُ»

“Muislamu hanajisiki”⁽¹⁸²⁾.

¹⁷⁷- Kitabu: [Wasaa'ilus Shii'a] cha Al-Hurrul 'Aamiliy (Jz. 6, Uk. 340).

¹⁷⁸- Kitabu: [Bihaar al-Anwaar] cha Al-Majlis (Jz. 5, Uk. 247-248).

¹⁷⁹- Surat Al-Muddathir/38

¹⁸⁰- Surat Al-An'aam/164.

¹⁸¹- Kitabu: [Al-Anwaar Nnu'maaniyyah] cha Ni'matullahi Al-jazaairiy (Jz. 2, Uk. 306), na kitabu: [Haqqul yaqiin] cha Abdullaahi Shubbar (Jz. 2, Uk. 188).

¹⁸²- Kitabu: [Bukhari] (285) na [Muslim] (371).

Kwa hiyo muislamu ni twahara akiwa hai na baada ya kufa kwake. Na kumwaga damu ya muislamu ni haramu kwa kauli ya Mtume-Swala na Salamu zimshukie:-

«فَإِنَّ دِمَاءَكُمْ وَأَمْوَالَكُمْ وَأَعْرَاضَكُمْ عَلَيْكُمْ حَرَامٌ»

“Hakika damu zenu, mali zenu, heshima zenu, ni haramu juu yenu”⁽¹⁸³⁾.

Sheria ya kiislamu imekuja kulinda haki hizo, haupasi kuvunja isipokuwa kwa haki ya uislamu. Ama kuhusu kukaa motoni milele hiyo ni hukumu ya makafiri, washirikina na wanafiki siku ya kياما. Tunamuomba Allaah atukinge.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Shia akimwita shia mwenzie: (Ewe sunni), atafanyiwa ta’azir (kufanyiwa izara kwa kutiwa adabu), ambayo itamkomesha]⁽¹⁸⁴⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Riwaya hii inasisitiza chuki yao dhidi ya Ahlus Sunnah na kuwadharau kwao, mpaka imefikia lau shia alimuita mwenzie kwa jina la sunni pia ni kosa linalopelekea kuadhibiwa!

23- KHURAFAT (UWONGO) WA SHIA NA UZUSHI WAO

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** Kuna kundi la Malaika walizozana kuhusu jambo fulani, wakatafuta hakimku katika wanadamu, Allaah akapeleka wahyi akiwaambia: Chagueni (mtu katika wao), wakamchagua Ally Bin Abi Twalib]⁽¹⁸⁵⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Allaah amesema hali ya kuwasifu Malaika:

﴿لَا يَعْصُونَ اللَّهَ مَا أَمَرَهُمْ وَيَفْعَلُونَ مَا يُؤْمَرُونَ﴾

“Hawamuasi Allaah kwa anayo waamrisha, na wanatenda wanayo amrisha”⁽¹⁸⁶⁾.

¹⁸³- Kitabu: [Bukhari] (1652).

¹⁸⁴- Kitabu:[Hayaat al-Muhaqqiq Al-Karakiy wa-aatharuhu] (Jz. 6, Uk. 237).

¹⁸⁵- Kitabu: [Musnad Faatima] cha Hussein At Tuweisirkaani (Uk. 296).

¹⁸⁶- Surat At Tahriim/6.

Allaah amewasifu Malaika kuwa wametakaswa na Kutenda dhambi na kukosea, kwa hiyo haiwezekani kwao kugombana na kutafuta hakimu katika wanadamu

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Kuna punda anaitwa ‘Ufeir alimwambia Mtume-Swala na Salamu zimshukie-: Namtoa fidia baba yangu na mama yangu kwa ajili yako. Hakika baba yangu amenisimulia mimi, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa babu yake, kutoka kwa baba yake, kwamba Yeye alikuwa katika jahazi pamoja na Nabii Nuh, akasimama Nabii Nuh na kumuelekea kisha akaupangusa mgongo wake na akasema: “Atazaliwa kutoka katika mgongo wa punda huyu, punda ambaye atampanda bwana wa Manabii wote na wamwisho wao. Namshukuru Mola ambaye amenijaalia mimi kuwa ndiye punda huyo”]⁽¹⁸⁷⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Mtume-Swala na Salamu zimshukie-hahitaji kutolewa Ushahidi na punda kuhusu Utume wake, achilia mbali kwamba hayo ni maneno ya kutunga wala si hadithi ya Mtume-Swala na Salamu zimshukie-, na imedhihiri wazi wazi upumbavu wa matungaji wake, baina ya Nabii Nuh -alaihis Salaam- na Mtume Muhammad -Swala na Salamu zimshukie- kuna karne nyingi zimepita, hakuna anaejua ila Allaah.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Imamu Baqir alitengeneza tembo/ndovu wa udongo, kisha akampanda na kuruka nae mpaka Makka]⁽¹⁸⁸⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Huku ni kukanusha cheo cha Allaah na kupwekeka kwake katika kuumba (Rubuubiyyah), kwani anayehusika na kuhuisha na kufisha ni Allaah pekee, na hakuna yeyote katika viumbe wake aliyempata nafasi hiyo isipokuwa Nabii Isa-alais Salaam-, na hafanyi ila kwa idhini yake Allaah
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakuna katika mikojo wala mavi ya Maimamu chenye kuchukukiza, wala uchafu, au harufu mbaya, bali (hupatikana harufu nzuri) kama miski yenye harufu kali, atakayekunywa

¹⁸⁷- Kitabu: [Usuul al-Kaafi] cha Al-Kulein (Jz. 1, Uk. 237).

¹⁸⁸- Kitabu: [Madiinat al-Ma’ajiz] cha Hashim al-Bahraani (Jz. 5, Uk. 10).

mkojo wao, damu, au kula mavi yao, Allaah atamharamishia moto na itawajibika kumuingiza yeye peponi] ⁽¹⁸⁹⁾.

- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Mkojo wa mwanadamu na mavi yake, katika hali yoyote ni najisi, ni wajibu kujiepusha navyo na kujitakasa, yeyote atakayekunywa mkojo wa imamu, au kula mavi yao, atakuwa amekunywa na kula najisi. Na hawa shia ni kama alivyosema Allaah:

﴿وَمَنْ يُهِنِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِنْ مُكْرِمٍ﴾

“Na anaye fedheheshwa na Allaah hana wa kumhishimu” ⁽¹⁹⁰⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Mashuzi/Ufuso na mavi ya maimamu ni sawa na harufu ya miski] ⁽¹⁹¹⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Mfano wa riwaya hizi zinafahamisha namna gani akili zao zimefikia katika daraja sawa na wanyama, hawana akili wala hawatafakari, hali ya kuwa Allaah anasema:

﴿وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِي آدَمَ وَحَمَلْنَاهُمْ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ وَرَزَقْنَاهُمْ مِنَ الطَّيِّبَاتِ وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَى كَثِيرٍ مِمَّنْ خَلَقْنَا تَفْضِيلًا﴾

“Na hakika tumewatukuza wanadamu, na tukawadhalilishia wao wanyama wa barani (nchi kavu) wa kuwapanda na baharini vya kuwabeba, na tumewaruzuku vitu vitu vizuri vizuri, na tumewafadhilisha kwa fadhila kubwa, kuliko wengi miongoni mwa tulio waumba” ⁽¹⁹²⁾.

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Kuvaa viatu vyeusi kunasababisha mambo matatu. Nikasema: Ni mambo gani hayo? Akasema: Kunadhoofisha macho, kunarefusha dhakari, na kunarithisha huzuni] ⁽¹⁹³⁾.
- **Na wanasema:** [Hakika kuvaa viatu vya rangi ya njano kuna faida tatu: Kunalinda macho, kunarefusha dhakari, na kunaondosha huzuni] ⁽¹⁹⁴⁾.

¹⁸⁹- Kitabu: [Anwaar al-Wilayah] cha Mulla Zainul ‘Aabidiin Al-Kalbaaikani (Uk. 440).

¹⁹⁰- Surat Al-Hajji/18.

¹⁹¹- Kitabu: [Usuul al-Kaafi] cha al-Kulein (Jz. 1, Uk. 319).

¹⁹²- Surat Al-Israa/70.

¹⁹³- Kitabu: [Usuul al-Kaafi] cha Al-Kulein (Jz. 6, Uk. 465).

¹⁹⁴- Kitabu: [Al-Furru’ minal Kaafi] cha Al-Kulein (Jz. 6, Uk. 465).

- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Mfano wa riwaya hizi zinafahamisha juu ya kushikamana kwao mashia na desturi na ibada za Jaahiliyya.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Kula karoti kunalainisha figo, kunasimamisha dhakari, na kunasaidia katika jimai (tendo la ndoa)]⁽¹⁹⁵⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Lau riwaya hizi ingelikuwa ni sahihi, wangelizitaja weledi na mabingwa wa mambo ya tiba, na kuwafahamisha watu wenye udhaifu katika tendo la ndoa.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Hakika shetani anakuja kwa mwanamke na kukaa naye kama anavyokaa naye mwanaume, akafanya kama anavyofanya mwanaume, na anaoa kama anavyooa mwanaume (wa kibinadamu). Akaulizwa Abu Abdillaah: tutajuaje hilo? Akajibu: “Kwa kutupenda sisi na kutuchukia”; Atayetupenda sisi atakuwa ni tone la manii la mja (mwema), na atayetuchukia atakuwa ni tone la manii la shetani”]⁽¹⁹⁶⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Riwaya hizi zinatilia msisitizo juu ya kuwavunjia kwao heshima waislamu, na kuwatuhumu kwamba ni watoto wa zinaa, wanatokana na tone la mani. Na kwamba hakuna muislamu wa kweli, Aliye twahara isipokuwa awe shia Imaamiyyah Ithnaasharia.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Uchi ni aina mbili: (tupu ya mbele na nyuma), tupu ya nyuma tayari imestiriwa na makalio, kwa hiyo ukiweza kustiri dhakari na korodani, utakuwa umestiri uchi]⁽¹⁹⁷⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Hii ndio fiqhi ya shia Imaamiyyah, hawezi kufanya hivi isipokuwa yule asiye na dini, na anayeishi porini na wanyama. Ama hukumu ya kisheria inayojulikana kwa waislamu wote, ni kwamba: Tupu ya mbele na nyuma ni uchi, amba oni wajibu kujistiri.
- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Ama baki ya starehe kama vile kugusa kwa matamano, kukumbatia, kumwaga manii kwenye mapaja, si vibaya (hilo) hata kwa mtoto anayenyonya]⁽¹⁹⁸⁾.

¹⁹⁵- Kitabu: [Al-Furū' minal Kaafi] cha Al-Kulein (Jz. 6, Uk. 372).

¹⁹⁶- Kitabu: [Al-Furū' minal Kaafi] cha Al-Kulein (Jz. 5, Uk. 502).

¹⁹⁷- Kitabu: [Al-Furū' minal Kaafi] cha Al-Kulein (Jz. 6, Uk. 501).

¹⁹⁸- Kitabu: [Tahriiru al-Wsiila] cha Al-Khomein (Jz. 2, Uk. 221).

- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Uislamu uko mbali na matamanio haya ya kinyama, na uko mbali na Fatwa hizi za kishetani, ambazo hakusalimika hata mtoto mchanga anayenyonya asiye na hatia!.

➤ **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Inafaa kumuingilia mwanamke kinyume ya maumbile (tupu ya nyuma)]⁽¹⁹⁹⁾.

- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Allaah Ta’alaa anasema:

﴿فَإِذَا تَطَهَّرْنَ فَأْتُوهُنَّ مِنْ حَيْثُ أَمَرَكُمُ اللَّهُ﴾

“Wakishat’ahirika basi waingilieni kupitia pale pahali Alipowahalalishia Allaah”⁽²⁰⁰⁾.

Allaah ametuamrisha kuwaingilia wanawake katika sehemu ambayo ni sababu ya kupatikana mtoto, ambapo ni tupu ya mbele ya mwanamke.

Pia Allaah anasema:

﴿نِسَاؤُكُمْ حَرْثٌ لَّكُمْ فَأَتُوا حَرْثَكُمْ أَنَّى شِئْتُمْ﴾

“Wake zenu ni kama konde zenu. Basi ziendeeni konde zenu mpendavyo”⁽²⁰¹⁾.

Na konde hapo ni tupu ya mbele ya mwanamke.

Na Mtume-Swala na Salamu zimshukie- anasema:

«مَنْ أَتَى حَائِضًا، أَوْ امْرَأَةً فِي دُبُرِهَا، أَوْ كَاهِنًا، فَصَدَّقَهُ بِمَا يَقُولُ، فَقَدْ كَفَرَ بِمَا أُنْزِلَ عَلَى مُحَمَّدٍ»

“Mwenye kumwingilia mwanamke mwenye hedhi, au akamwingilia katika duburi yake (kinyume ya maumbile). Na kwenda kwa Kuhani (Mpiga ramli), akamsadikisha kile alichomwambia, huyo ameyakanusha yale aliyo teremshiwa Mtume Muhammad -Swala na Salamu zimshukie-”⁽²⁰²⁾.

Pia amesema:

«مَلْعُونٌ مَنْ أَتَى امْرَأَتَهُ فِي دُبُرِهَا»

“Amelaaniwa Mwenye kumuingilia mke wake nyuma (kinyume ya maumbile)”⁽²⁰³⁾.

¹⁹⁹- Kitabu: [Al-Furuu’ minal Kaafi] cha Al-Kulein (Jz. 5, Uk. 540).

²⁰⁰- Surat Al-Baqara/222.

²⁰¹- Surat Al-Baqara/223.

²⁰²- Kitabu: [Sunan Tirmidh] (135) na [Sunan Ibn Majah] (639).

²⁰³- Kitabu: [Sunan Abi Daud] (9731) na [Musnad] (9731).

- **Shia Ithnaasharia wanasema:** [Inajuzu kwa mwanamke mwenye hedhi kuswalia maiti, lakini asipange safu pamoja na wenzie]⁽²⁰⁴⁾.
- **Na sisi Ahlus Sunnah tunasema:** Mwanamke mwenye hedhi haruhusiwi kufunga wala kuswali, kwa sababu miongoni mwa masharti ya swala ni twahara, akipata hedhi itakuwa imekosekana sharti moja miongoni mwa masharti ya swala, nalo ni sharti la kuwa twahara.

Huu ndio mwisho wa kile nilichokikusanya, katika kuoanisha baina ya itikadi za Waislamu wa Kisunni (Ahlus Sunnah), na itikadi za Shia Ithnaasharia, na imebainika wazi ndani yake, kwamba dini ya Shia ni imejipenyeza katika dini ya Kiislamu, na kwamba misingi yake ya Kiimani, Itikadi na hukumu zake ni tafauti na Itikadi na hukumu za Kiislamu.

Swala na Salamu zimshukie Mtume wetu Muhammad, Jamaa zake, na Maswahaba wema.

Abdullaah Bin Muhammad As Salafiy

20/Jumaadal Uulaa/1440h.

²⁰⁴- Kitabu: [Man laa yahdhuru al-Faqiih] cha Ibn Baabawaihi al-Qummi (Jz. 1, Uk. 179).